**30 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 30 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

Na. 483

**Serikali Kutekeleza Ahadi ya Rais**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Kiwira Jimbo la Rungwe litatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepeleka kwenye halmashauri ya Wilaya ya Rungwe shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Iponjola na Kituo cha Afya Ndanto ambapo ujenzi wa Vituo hivi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Afya kwenye Kata ya Kiwira. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nilikuwa ninaomba kuuliza swali; Kata ya Kiwira ina wakazi/wananchi wa pale zaidi ya 40,000 na sasa hivi kuna zahanati ambayo inahudumia wagonjwa 300 mpaka 400 kwa siku na hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ambapo kituo cha afya hicho kikijengwa kingeweza kusaidia kata jirani kama Kata ya Swaya, Ikunga, Lupepo na Kinyala.

Sasa je, ni lini Serikali itakwenda kutimiza ahadi hiyo ya ujenzi wa Kituo cha Afya pale kwenye Kata ya Kiwira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kata ya Kisondela ina hospitali kubwa sana ambayo ilifungwa miaka 20 iliyopita iliyokuwa ikihudumia wagonjwa wa ukoma.

Sasa je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa majengo hayo ambayo ni mengi ambayo yangesaidia kutibu wagonjwa ambao wanakaa kwenye Kata ya Kisondela, Mpuguso, Ilima na Malindo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Fyandomo ambaye ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Mwantona kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimuhakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni Serikali sikivu na ndio maana alipokuwa kwenye kampeni pale Kiwira alitoa ahadi ya kuleta kituo cha afya na nikuhakikishie kwamba kwenye mwaka ujao wa fedha 2022/2023 tumetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuhakikisha sasa tunajenga kituo cha afya ili wananchi hawa zaidi ya 40,000 wapate huduma bora za afya pale Kiwira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo limeshafanyiwa kazi, lakini kuhusiana na hospitali hii ya wagonjwa wa ukoma ambao imefungwa miaka mingi iliyopita tutakwenda kufanya tathmini tuone gharama zipi zinahitajika kufanya matengenezo na ukarabati ili iendelee kutoa huduma za afya kwa wananchi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Kata ya Endagaw, Wilaya ya Hanang haina kabisa huduma ya afya; je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri ya Hanang tumeweka mpango mkakati wa kuainisha maeneo ya vipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati. Kwa hivyo, tutakwenda kulipitia eneo hilo kama linakidhi vigezo tutakwenda kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi.

Kituo cha Afya Kabwe ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunashukuru kwamba Serikali imetuletea fedha, lakini fedha ile haiwezi kumaliza hicho kituo cha afya. Ni lini sasa mtatuletea fedha iliyobaki ili kuweza kukamilisha hicho kituo cha afya kisaidie Kata ya Korongwe na Kabwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kituo cha Afya cha Kabwe kilipelekewa fedha na tunajua kwamba tunajenga vituo vyetu vya afya kwa awamu kwa awamu ya kwanza tayari ujenzi unaendelea, lakini tukuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nkasi Kaskazini kwamba Serikali itapeleka fedha awamu ya pili ili kukamilisha majengo yale ambayo yamebakia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza.

Jimbo la Tabora Mjini lenye Kata 29 tuna ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Tumbi ambao haujakamilika. Sijui Serikali ina mpango gani wa kuleta fedha za kukamilisha kituo hicho cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo hivi vya afya ambavyo tayari ujenzi umeanza tumeanza hatua ya kwanza tukumbuke kwamba Vituo vyote hivi tunajenga kwa awamu ya kwanza shilingi milioni 250, awamu ya pili shilingi milioni 250 kukamilisha awamu ya kwanza sasa ya ujenzi wa vituo hivi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaleta fedha kwa awamu ya pili kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya ambacho kinaendelea na ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 484

**Idadi ya Watumishi *TARURA* – Kilimanjaro**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza watumishi wa kada ya uhandisi na fundi sanifu *(technicians)* kwa *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Dkt. Dugange ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro ina wahandisi 18 na upungufu wa wahandisi wanne na mafundi sanifu sita. Serikali imepeleka wahandisi watatu katika Mkoa wa Kilimanjaro walioajiriwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuwezesha upatikanaji wa vibali vya ajira za watumishi wa kudumu na hivyo kuweza kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi katika Mkoa wa Kilimanjaro na Mikoa mingine nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bushiri nakuona umekaa halafu kama unataka kusimama. Mheshimiwa Bushiri swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya zote saba zina upungufu wa watumishi katika kada hizi za *engineer* na *technician*. Kwa kuwa kada hizi ni muhimu sana katika ujenzi, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuongeza ajira katika kada hizi ili kupunguza upungufu uliopo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kazi njema anayofanya Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro ya kufuatilia maeneo hayo ambayo ameainisha hapo na sisi

tunaona umuhimu kama Serikali ya kuongeza ajira hususani kwa wahandisi na mafundi sanifu katika maeneo yote nchini. Kwa hiyo, jambo hilo tumelipokea na tutaomba kibali Ofisi ya Rais, Utumishi ili sasa tuweze kupatiwa na kuajiri ili tuongeze watu hao kwa ajili ya ujenzi nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi.

Pamoja na jitihada za Serikali zilizofanywa za kupeleka fedha za *TARURA* Wilaya ya Katavi na Wilaya ya Tanganyika, lakini kuna upungufu mkubwa sana wa tatizo la vitendea kazi kama magari kwa wafanyakazi wa *TARURA*.

Je, ni lini Serikali itapeleka magari kwenye eneo la Mkoa wa Katavi hasa Wilaya ya Tanganyika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tutaleta magari kwa sababu Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* tumeagiza magari kwa ajili ya halmashauri zote nchini na baadhi ya halmashauri zimeanza kupokea. Kwa hiyo, tutafikisha na huko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni *TARURA* walikuwa na Mameneja kila halmashauri lakini sasa hivi wameondoa utaratibu huo wameweka kila wilaya.

Je, TAMISEMI/Serikali hamuoni kwamba mnapunguza utendaji kazi kwa nini msirudishe wale Mameneja wa halmashauri ili halmashauri zikapata kusimamia barabara na miundombinu ya *TARURA* kwa ukaribu zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Taasisi yake ya *TARURA* tulitengeneza muundo mpya na muundo mpya ni kwamba una Mameneja katika ngazi ya wilaya na sio katika ngazi za halmashauri. Lengo kubwa lilikuwa ni kuongeza ufanisi, lakini vilevile kupunguza gharama katika uendeshaji kwa hiyo, tunataka tuangalie huu muundo mpya utakavyofanya kazi na mara baada ya hapo tutafanya tathmini mpya kama kuona kuna namna ambayo inaweza kutuwezesha kurudi kule. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa vile ngazi hii ya mafundi sanifu ndiyo muhimu sana katika sekta zote za ufundi nchini *TARURA* ni

mojawapo. Serikali ina mpango gani wa kuzalisha mafundi sanifu ili kukidhi mahitaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia moja ya mpango wake ni kuhakikisha kwamba vyuo vya elimu ya kati vinaboresha zaidi hawa mafundi sanifu na ndiyo mpango uliopo wa Serikali. Kwa hiyo, kadri vyuo vinavyoongezeka na wanavyoongeza udahili maana yake tutakuwa na idadi nzuri inayoridhisha kwa ajili ya Mafundi Sanifu watakaosaidia katika sekta yetu hususani ujenzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ilipanga vijana waliomaliza kidato cha nne kwenda kidato cha tano na wengine kwenda vyuo, lakini imetokea kwamba watoto waliomaliza kidato cha nne wenye *division one* na *division two* wamefaulu vizuri masomo ya sayansi wamepelekwa kwenye hivi vyuo vya kati bila wao kupenda na wakiomba kubadilisha kwenda kidato cha tano inakuwa *procedure* ni ndefu.

Ni kwa nini utaratibu huu usibadilishwe ili baada ya kutoa kidato cha tano wanaobaki kwenda kwenye hivi vyuo vya kati wachague wenyewe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza naomba nisahihishe Mheshimiwa Mbunge alichokisema, hakuna mwanafunzi ambaye amepelekwa chuo cha kati bila yeye mwenyewe kuomba. Kwa sababu kwenye mfumo wote waliomba sasa kuna makosa ambayo yalikuwa yamefanyika kwa watoto wenyewe ambao wengine walijaza chaguo la kwanza kwenda vyuo vya ufundi halafu wakawa wamefaulu baadaye wakawa wanataka kubadilisha kwenda hatua ya pili na sisi tuliruhusu hiyo *room* ya wanafunzi wote wanaotaka kubadilisha waje Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafanya hilo jambo. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Serikali hatukufanya hilo kwa kuwapeleka watoto wa *division one* na *division two* kwa makusudi mifumo ipo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane Mbunge wa Kilwa Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 485

**Kudhibiti Tembo katika Kata za Kandawale na Miguruwe – Pori la Akiba Selous**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti tembo wanaoharibu makazi na mashamba katika Kata za Kandawale na Miguruwe ambazo zinapatikana na Pori la Akiba Selous?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara imeanza kujenga vituo vya askari wanyamapori katika maeneo mengi nchini kwa lengo la kuwa karibu na wananchi ili kuwadhibiti wanyama hao. Aidha, Wizara imepata kibali cha kuajiri askari 600 ambao watasambazwa kwenye maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea na zoezi la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu za kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Katika Kijiji cha Ngalambilyenga kule kwa Kinjeketile Ngwale tarehe 27 Juni, 2021 saa 5.00 asubuhi tulimpoteza mwananchi mmoja anayejulikana kwa jina la Alhaji Chande Ngambumage, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, lakini sasa ni mwaka mmoja tangu yule mwananchi alipofariki lakini familia yake haijalipwa fidia ya shilingi milioni moja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha *process* za ulipaji wa fidia hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini atafika katika Wilaya ya Kilwa ili tuweze kushirikiana na wananchi wa Wilaya ya Kilwa katika kudhibiti wanyamapori hawa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapa pole sana wananchi wote walikokutana na kadhia hii ikiwemo kupoteza maisha, Serikali inatambua changamoto hizi lakini hata sisi pia hatufurahii na changamoto hii hasa inapofikia mahala tunapoteza maisha ya wananchi. Hivyo nawapa pole sana wananchi wa Ngalambi.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kifuta machozi tutaenda kulishungulikia na kuhakikisha kwamba wananchi

hawa wanalipwa kwa wakati. Niombe tu Waheshimiwa Wabunge changamoto tunayoipata ni kwamba kuna ucheleweshwaji kati ya mawasiliano kutoka kwenye halmashauri ambazo zitakwenda kufanya tathmini kutuletea sisi ili sisi twende kulipa kifuta machozi ama kifuta jasho. Hivyo niwaombe kushirikiane kuhakikisha orodha za hawa wenye madai zitufikie kwa haraka ili tuweze kukamilisha zoezi hili kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lini nitafika Kilwa nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba itafanya ziara huko ili kuzungumza na wananchi, lakini pia kuwapa pole na changamoto hii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani kuja kutusaidia na sisi wananchi wa Kidugale kuwatoa hawa tembo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taletale kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Taletale, tulishapanga kufanya ziara katika jimbo lake, nimuahidi tu kwamba tutafika baada la Bunge hili kuisha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Katika Kata za Lunguza, Mng'aro na Mnazi ambazo ziko pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa Mkomazi tembo wamekuwa wakivamia kila siku hata leo walikuwepo.

Je, katika hivi vituo ambavyo vitajengwa na sisi tutabahatika kupata kituo kimoja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vya Lunguza Mng'aro na Mnazi tumepanga kupeleka kituo cha askari wa wanyamapori ili kudhibiti maeneo hayo ambayo iko kando kando na hifadhi ya mkomazi. Hivyo nimuhakikishie tu Mbunge kwamba suala hili tumeanza kulishughulikia tuna vituo 19 nchi nzima kwa mwaka huu wa fedha ambao unaisha leo na kuanzia tarehe 1 Julai tuna vituo 13 vya nyongeza ambavyo tunaenda pia kuvijenga ikiwemo hawa askari 600 ambao tumepata kibali kutoka kwa Mheshimiwa Rais. Hivyo niwahakikishie wabunge kwamba tunaenda kusambaza vituo vingi katika maeneo yenu ili kudhibiti wananyama wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Je, Serikali haioni haja ya kuja Wilaya ya Meatu kuja kuona uharibifu mkubwa uliofanywa na tembo kwenye

mashamba ya wananchi yenye mizinga ya nyuki, uharibifu mkubwa umefanywa kuliko hata maeneo yale ambayo hayana mizinga ya nyuki ili kuweza kuona jinsi wananchi walivyokosa mavuno nawengine zaidi wameuwawa katika kipindi hiki kifupi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Meatu kwamba tutafika kufanya ziara hiyo na hivi ninavyoongea tayari vituo vilishaanza kujengwa hilo Mbunge analifahamu, lakini wananchi pia wa Meatu niwahakikishie kwamba Serikali itafika katika maeneo hayo ili kutoa pole lakini pia kutoa ufafanuzi wa namna ya kujikinga na wananyama wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika Kata ya Mbati na Malumba tembo wameweka kambi kwa muda mrefu sasa katika vijiji Misaje, Mbati yeneywe, Marumba, Mpanji, Molandi pamoja na Mchoteka.

Je, Serikali inampongo gani wa kujenga kituo katika Kata hizo ili kudhibiti makambi haya ya tembo ambayo yanaendelea kila mwaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Mpakate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kujenga vituo kwa ajili ya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu ni jukumu la Serikali na tumshukuru Mheshimiwa Rais kwamba aliliona baada ya kuona changamoto hii imeongezeka. Nimakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi walioko katika maeneo haya tutahakikisha kwamba tunajenga kituo kimoja ili iturahisishie kudhibiti tembo katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitoe maelekezo, Mheshimiwa Mbunge amesema kuna tembo wameweka kambi katika maeneo hayo, nielekeze askari walioko Nyanda za Juu Kusini waende katika maeneo hayo ili kwenda kuwatoa wale tembo na kuwarudisha hifadhini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti tembo na kuwalipa fidia wananchi wa kata ya Mboliboli, Pawaga, Isimani ambapo hivi karibuni wameuwa watu wawili na kuaribu mazao yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama hatujapata orodha ya madai ya watu ambao wamekutana na changamoto hii ni ngumu sana sisi kufahamu, nimeomba ikiwezekana tushirikiane na

Waheshimiwa Wabunge na halmashauri kwa sababu hawa wananchi wanapokutana na kadhia hii watu wa kwanza kwenda kufanya *evaluation* ni halmashauri, halmashauri inatuletea idadi ya wananchi wanaodai kifuta machozi na kifuta jasho na tunapopata ile orodha sisi ndiyo tunapeleka fedha kwa ajili ya kulipa hawa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo niwaombe tushirikiane kuzipata hizi orodha ambazo zinaonekana sisi tunaona tumelipa kumbe kwa upande wa pili bado wananchi hawajalipwa. Niwaombe hizi orodha tuzipate ili wananchi walipwe kwa wakati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Changamoto ya tembo kuingia kwenye maeneo ya watu na kuua wanyama iko pia katika wilaya ya Karatu katika Kata Olidian, Nganakorote na Mbulu mbulu na wiki iliyopita tum wananchi mmoja ameuwawa kwenye kata ya Olidian.

Je, Serikali inamkakati gani wa kudhibiti tembo hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyonge la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Karatu ni kweli kumekuwa na changamoto ya wanyama wakali na

waaribifu, wananchi wa Karatu tunawapa pole, lakini niendelee kuomba tu kwamba orodha hizi tuzipate kwa wakati ili tuweze kuwalipa wananchi hawa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MBUNGE FULANI:** Hajasimama *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Nani hajasimama, alishasimama mwanzo, kwa hiyo ninayo orodha hapa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ngoja ngoja, hajasimama sasa, lakini ninayo orodha ya Wabunge wote ambao wamesimama na ambao nitawapa nafasi, tumeelewana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsate, naomba kuuliza swali; kwa kuwa Jimbo la Bunda kwenye *graph* na kwenye *data* zinazoonesha ndiyo jimbo linaloathirika na tembo hapa Tanzania.

Ni lini sasa vituo vya kuzunguka Mto Lubana vitajengwa ili kuzuia tembo kabla hawajafika kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye maswali ya msingi kwamba Serikali ina mpango wa kujenga vituo vingi katika maeneo mengi yenye changamoto ya wanyama wakali na waharibifu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Getere kwamba wananchi wa Bunda katika maeneo ya Lubana tutaangalia uwezekano huo, lakini pia eneo hili tumeshailekeza Serikali ya Mkoa kwamba kuna mchakato ambao unaendelea wa kupisha maeneo hayo.

Kwa hiyo, kuna baadhi ya shoroba ambazo tumeshaainisha ambazo tunaona hata kama tukijenga vituo vya askari ni ngumu kuwadhibiti hawa tembo. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo tutahakikisha kwamba wananchi wanapisha hizi shoroba ili kuwe na uwezekano wa wanyama kwenda kupata huduma ambazo zinastahili. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Getere maeneo yale ambayo hayatahusisha shoroba tutapeleka vituo vya askari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa suala la tembo kuharibu mazao ni la kila msimu wa kilimo hasa katika Kata za Bagugu, Galapo na Mwada katika Jimbo la Babati Vijijini. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kudhibiti tembo hawa ili wasiendelee kuharibu mazao ya wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto hasa za kipindi cha mavuno, wanyama wakali na waharibifu huwa wanaenda kwenye mashamba ambako wananchi wamelima mazao yao na kushambulia maeneo hayo. Tuna mpango wa muda mrefu na wa muda mfupi; mpango wa muda mrefu ni kuhakikisha shoroba ambazo zimevamiwa wananchi wanaziachia, lakini mpango huu utakuwa ni wa muda mrefu. Mpango wa muda mfupi ni kuweka vituo vya askari katika maeneo hayo ili kudhibiti tembo hao.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kukabiliana na changamoto hii lakini kwa wakati huo huo tunaangalia namna iliyobora ya kuruhusu maeneo ya mapito ya wanyama yaachiwe ili shughuli za kibinadamu zifanyika katika maeneo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo pia yanaathirika sana na wanyama tembo ni pamoja na Jimbo la Bunda Mjini hasa maeneo ya Mihale, Luzungu, Nyamatoke, Nyatwali, Tamau na Serengeti.

Nilitaka kujua ni lini mtaongeza askari na magari ya *patrol* ili wananchi wa maeneo haya waondokane na adha ya kuharibiwa mazao yao na tembo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Ester Bulaya, ndugu yangu Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tu wananchi wa Bunda kwamba suala hili tumeshalipata, tulishalipokea Mheshimiwa Ester amekuwa akiliongelea sana Bungeni, lakini pia na Mheshimiwa Mbunge amekuwa pia akiliongelea sana, tutahakikisha tunaimarisha maeneo haya ili wananchi waweze kuishi ikiwemo kuweka vituo vya askari ili kudhibiti hawa wanyama wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Katika Jimbo la Manyoni Magharibi linapakana na mapori ya akiba ya Rungwa na Muhesi, sasa tembo wanaotoka katika mapori haya wanahamia hata katika vijiji vya kwenye Kata ya Kitaraka, Kijiji cha Kitaraka chenyewe, Kaskazi na Kata ya Aghondi katika vijiji vya Kamenyanga na Njirii.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuwadhibiti hawa tembo maana yake wamekuwa kero kubwa na muda mrefu sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto katika maeneo haya hasa kwenye mashamba ya korosho ambako wanyama wakali na waharibifu wamekuwa

wakiingia katika mashamba hayo. Tumeshagundua shoroba zake na hivi ninavyoongea tumewaelekeza askari na wameendelea kuangalia namna iliyobora ya kudhibiti maeneo hayo.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili limeshatufikia tunaendelea kulishughulikia ili kudhibiti wanyama hawa ili waweze kurudi katika pori la Rungwa ambako ndiko hasa halisi ya makazi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi sana nchini ya wananchi kuvamiwa na tembo.

Je, Serikali haioni wakati muafaka sasa umefika wa kuvuna tembo hao kwa utaratibu ambao umejipangia ama utaratibu ambao unafaa ili kupunguza vifo na madhara yatokanayo na uvamizi wa tembo hawa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kutoa ufafanuzi kwamba kumekuwa na dhana ya watu wengi wanaamini kwamba hawa wanyama wameongezeka, lakini tukumbuke kwamba hawa wanyama kabla ya kipindi hiki walikuwa wanateseka sana na walikuwa wanachangamoto ya ujangili. Kwa utafiti ambao watalaam wameshafanya wanatuelezea kwamba hawa Wanyama mpaka sasa idadi yao haijafika hata idadi yam waka 2009 ambao wanyama hawa walikuwa

134,000 na kwasasa wanakadiriwa kuwa 55,000 mpaka wana *range* kwenye 60,000.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi ambao tunapenda kuwaambia wananchi ni kwamba kwa kuwa tumekuwa na ongezeko la wananchi ambao wamekuwa wakiendelea kusogea kwenye maeneo ya hifadhi, lakini wakati huohuo kuna shughuli za kibinadamu na ukiangalia kipindi cha malalamiko ya tembo ni kipindi cha kuanzia mwezi wa nne mpaka wa saba ambapo ndiyo kipindi cha mavuno. *Research* inatuambia kwamba hawa wanyama huwa wananusa takribani kilometa 200 ananusa harufu ya kinachom-*face*. Kwa hiyo, sisi tunaamini kwamba mazao yanapokuwa katika hatua ya kukamilika kuvunwa hawa tembo wanahamasika kwenda kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, si kwamba kweli hawa tembo wameongezeka, isipokuwa shughuli za kibinadamu zimeongezeka.

Mheshimiwa Spika, tuongee bila kumung'unya kwa sababu tunataka tuingize siasa kwenye hawa Wanyama, ni kwamba shughuli za kibinadamu zimeongezeka ndiyo changamoto za tembo nazo zimeongezeka ikiwemo shoroba zimezibwa kwaajili ya shughuli za binadamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa kifuta machozi wanachopewa waathirika wa wanyama waharibifu ni kidogo sana. Ni lini Serikali itakuwa tayari kuipitia kanuni ya kifuta machozi ya mwaka 2011 ili iendane na mazingira tuliyokuwa nayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge wa Korogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshapokea malalamiko haya kwamba ni kweli ukiangalia kiwango tunachowalipa hawa wananchi hakifanani na uhalisia wa gharama na hata mazao ambayo yameliwa. Tumeshapokea haya maombi na tunaingiza kwenye mchakato, tutaleta katika Bunge lako hili ili Wabunge hawa hawa wapitishe mabadiliko ya sheria hii ambayo tuliipitisha humu humu ndani ili tuweze kuongeza kiwango hiki kwa ajili ya kukidhi haja za wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika Mkoa wetu wa Iringa, Wilaya ya Kilolo katika Kata ya Ruaha Mbuyuni, Nyanzwa, Mahenge wananchi wamekuwa wakipata uharibifu mkubwa sana wa kuharibiwa mazao yao na tembo na fidia hawapati.

Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari sasa kuja kujionea mateso makubwa wanayopata wananchi wa Wilaya ya Kilolo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi ni nyingi, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Ritta Kabati kwamba Wizara pamoja na Mheshimiwa Waziri tutapita katika maeneo hayo kutoa pole, lakini pia kuzungumza na wananchi, lakini pamoja na hayo tumekuwa na bidii za kuelimisha wananchi namna ya kujikinga na wanyama wakali na waharibifu. Hivyo nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge tutaleta watalaamu wa kufundisha wananchi, lakini na sisi tutafika katika maeneo hayo kuzungumza na wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba shughuli za wananchi zimeongezeka na tembo hawa wanafuata mazao.

Sasa ni kwanini Serikali isione mbadala wake wakalima hayo mazao kama ni matikiti na mahindi ili hao tembo waweze kuwa wanaenda kulishwa kwenye hifadhi kuliko kwenda kuvamia kwa wananchi? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kutunza maeneo yaliyohifadhiwa na haya maeneo yaliyohifadhiwa tunayaita ni ya Serikali, lakini kwa asilimia mia moja ni kwa faida ya wananchi. Kwa hiyo, tunapokuwa tunayatunza, tunahakikisha wananchi wanapata huduma mbalimbali

kutoka katika maeneo hayo ikiwemo kupata hewa safi, mazingira safi, mvua ziweze kunyesha ili wananchi waweze kulima mazao yao, lakini wakati huo huo wanapata wadudu wanaohifadhiwa kwenye hifadhi waweze kuchavusha mazao kwenye maeneo yao ambayo wanafanya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tunapotaka kulima sasa kuhakikisha tulime ndani ya hifadhi, kwanza tutaharibu mazingira ya uhifadhi, lakini pia hata ule uoto wa asili ambao tunautunza tutaenda kuuharibu. Kwa hiyo, *meaning* ya uhifadhi itakuwa haipo, lakini pia tukumbuke kwamba hizi hifadhi zimo kwenye mikataba ya *UNESCO* ambayo ndani yake kuna hifadhi mbalimbali katika mataifa mngine.

Kwa hiyo, sisi tunatunza kwaajili ya faida ya kizazi cha leo na kijacho. Sisi tuendelee kuwaomba wananchi kwamba mita 500 kutoka kwenye hifadhi ziachwe kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ili wasiendelee kusogelea kwa sababu ukiangalia changamoto hii unakuta kigingi kipo hapa kwenye hifadhi, halafu mwananchi ameenda kulima pembeni ya kigingi, halafu anakuja anaidai Serikali kwamba naomba nilipwe fidia, utaona kabisa kwamba umelima kwa ajili ya wanyama wale na tunajua kwamba hata mifugo ya nyumbani hatupitishi kwenye maeneo hayo kwa sababu tunaogopa ng'ombe na kadhalika wakipita maeneo wanaweza wakashambulia mazao.

Kwa hiyo niwaombe wananchi tuendelee kuheshimu maeneo ya hifadhi na tusilime kandokando ya hifadhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtakubaliana nami Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu maswali yenu mengi sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Neema Wilium Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 486

**Kujenga miundombinu rafiki kwa wafanyabiashara na wavuvi wa samaki – Ludewa**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itajenga miundombinu rafiki ya kufanya biashara ya samaki pamoja na kuhifadhia vifaa vya uvuvi yaani mwalo katika Kata ya Ruhuhu iliyopo Wilayani Ludewa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023 Wizara ya Mifugo na Uvuvi itatuma wataalam wake Wilayani Ludewa ili kufanya upembuzi yakinifu wa athari za mazingira na jamii wa maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu rafiki ya uvuvi ikiwemo mialo, masoko, maghala na sehemu za kuhifadhia vifaa vya uvuvi. Lengo ni kuwawezesha wavuvi na wafanyabishara wa samaki na mazao ya uvuvi wa Wilaya ya Ludewa ikiwemo Kata ya Ruhuhu kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kwa tija.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi hilo kukamilika, Wizara itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kuanza ujenzi wa mwalo mmoja katika eneo litakaloonekana

linafaa Wilayani Ludewa na ambalo wananchi wataridhia kutoa eneo hilo la ardhi bila ya fidia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nitamuuliza maswali mawili ya nyongeza; kwa bajeti hii nzuri ya kwanza ya Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, je, kuna fursa gani ambazo zitakwenda kuwanufaisha wavuvi na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, upo tayari kuongozana na mimi pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ludewa kwenda kuona wavuvi wetu wanavyotumia zana duni katika shughuli za uvuvi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni juu ya fursa zitakazowanufaisha wavuvi na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi kulingana na bajeti hii ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono na maelekezo yake kupitia bajeti hii ya wananchi ya mwaka 2022/2023 ambapo kwa mara ya kwanza sekta ya uvuvi imepata kipaumbele kikubwa sana, hasa hususani wavuvi wadogo wadogo ambapo miongoni mwa fursa hizo ni pamoja na kutengwa pesa kwa kushirikiana na Benki ya

Kilimo, boti zaidi ya 300 zitakopeshwa kwa wavuvi hususani wavuvi wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia fursa zingine ni pamoja na kuanzishwa kwa viatamizi vya ufugaji wa Samaki, ambapo zaidi ya viatamizi 246 vitakavyochukuwa vijana wasiopungua 1000 katika Ziwa Victoria, watafunzwa kufanya kazi ya ufugaji wa samaki. Matarajio yetu ni zaidi ya tani 8,000 kuzalishwa kutoka katika viatamizi vile ambavyo vitakuwa na thamani ya samaki wasiopungua bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, pia vilevile katika bajeti hii tumetenga pesa kwa ajili ya halmashauri mbalimbali kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji wa samaki ambayo haya yatakwenda kuwanufaisha vijana na akina mama. Lakini kwa upande wa wafanyabiashara kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge yapo marekebisho ya tozo, mfano tozo za uagizaji wa samaki aina ya *crustacean* na *cephalopods* yaani kaa, kambakochi na pweza wanaotoka nje ya mipaka ya nchi yetu ambao hao kwa kawaida uwa wanaagizwa na baadhi ya wafanyabiashara hapa nchini kwa lengo la kuwachakata na kuwasindika na kuuza nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tozo hizi tumezipunguza kupitia jedwali la marekebisho ya tozo kutoka dola 2.5 mpaka dola 0.5 ili kufanya urahisishaji wa ufanyaji wa biashara na fursa nyingine ni ile iliyokuwa ikilalamikiwa na wafanyabiashara wengi wa mazao ya uvuvi ambapo leseni za kufanya biashara zilikuwa nyingi na kwa hivyo sasa tumekubaliana kuunganisha leseni hizi, kwa mfano, mfanyabiashara wa mazao ya dagaa wakavu na wabichi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna Wabunge wengi walisimama hapa kwa ajili ya kukuuliza maswali ya nyongeza, kwa hiyo fupisha kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, wafanyabishara hao tumekubaliana kwamba leseni zile sasa tunaziunganisha ili ziwe moja ili kuwaondolea mlolongo wa leseni nyingi.

Swali lake la pili ni juu ya ziara, Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Ludewa niko tayari baada ya Bunge kuweza kuunganisha ziara ya kuweza kwenda kule Ludewa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Wilaya ya Kigamboni ina uwanda wa bahari wa takribani kilometa 70 na asilimia 90 ya wavuvi wote wa Mkoa wa Dar es salaam wanatoka Wilaya ya Kigamboni?

Je nini mpango wa Serikali wa kujenga soko kubwa la kisasa la samaki katika Wilaya ya Kigamboni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvivu, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Serikali imetenga fedha kwa ajili ujenzi wa soko katika Wilaya ya Kigamboni kama ambavyo limeombwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, je Serikali ina mpango gani wa kushajihisha na kufundisha ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba ili kuongeza mazao katika mito na maziwa yetu ambayo tumebarikiwa kuwa nayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvivu, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Juma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kujibu katika jibu la msingi tayari katika bajeti yetu ya mwaka 2022/2023 tumetenga pesa kwa lengo la kuweza kuwezesha ufugaji wa samaki na kwa hivyo mpango huu tunao na tutaendelea nao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, kwa kuwa sisi Wilaya ya Namtumbo tuna mito ambayo iko katika Hifadhi ya Selous au ya Mwalimu Nyerere Mto Londo, Mbaran'gandu Likuyu, Lutukira, Luwegu na Mto Ruvuma; na ina samaki wengi sana, lakini wananchi hawaruhusiwi kuvua samaki hao.

Je, Serikali inaweza kuruhusu wananchi kwa utaratibu maalum kuvua samaki hao kuliko kuachwa wazaliwe, wazeeke na wafie majini bila binadamu kuwavua na kuwala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvivu, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo aliyoyataja ni maeneo ya hifadhi yanayohifadhiwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, na kwa hiyo ombi lake la kwamba tuwe na utaratibu maalum ni mazungumzo na ni mchakato baina ya Wizara hizi Serikalini kuona kama jambo hilo linawezekana kufanyika kivitendo. Lakini kwanza ni maeneo ya hifadhi na yanalindwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wetu wengi wa samaki mfano Soko Kuu la Musoma na kule Soko la Saanane pamoja na masoko mengine nchini wanapata hasara ya kufanya biashara ya samaki kwa sababu wale samaki wanaharibika baada ya siku moja.

Je, ni lini Serikali sasa itawawekea miundombinu ya majokofu katika masoko yetu ili wafanyabiashara wetu wasiendelee kupata hasara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo programu katika bajeti hii ya mwaka 2022/2023 ya kuweza kupunguza upotevu wa mazao

ya samaki kwa maana *postharvest loss* kwa kujenga vichanja, lakini pia kupata *cold rooms* na halikadhalika kupata mashine maalum za ukaushaji wa dagaa. Programu hii tunaendelea nayo na yawezekana baadhi ya maeneo aliyoyataja yakaweza kunufaika katika programu hii ya Serikali. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa. Idadi ya samaki katika Bwawa la Nyumba la Mungu imepungua sana.

Je, Serikali ina mpango gani kusaidia wavuvi wanaofanya biashara ya samaki kukabiliana na changamoto hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Nyumba ya Mungu kutokana na wingi wa watu na wingi wa mahitaji idadi ya samaki imepungua na hivyo sasa hapa ni mambo makubwa matatu ambayo tunaweza kuyafanya; la kwanza ni kudhibiti uvuvi haramu kwa pamoja na mamlaka zinazohusika za kule wilayani; lakini pia vilevile jambo la pili *TAFIRI* tunawaelekeza kuona uwezekano wa kupandikiza zaidi samaki na kupeleka programu ya vizimba ili wananchi wale waweze kunufaika na rasilimali hizi za samaki. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; miundombinu ya kukaangia samaki ni muhimu ili kulinda afya za walaji, wakaangaji na mazingira. Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu hiyo katika Soko la *Ferry* Mtwara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Agnes Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juu ya usalama wa chakula na kutengeneza miundombinu rafiki kama nilivyokwisha kujibu katika jibu la msingi, ni kwamba tunayo programu na bajeti imetengwa, baadhi ya maeneo yatanufaika. Na kwa hiyo, nimelichukua hili la Mtwara Mikindani na kwenda kulifanyia kazi kuona uwezekano kama Soko la Mtwara Mikindani na lenyewe linaweza kuwa ni sehemu ya yatakayofaidika katika programu hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba niulize Serikali; ni lini itapeleka majokofu ya kuhifadhia samaki ambao wanaendelea kuharibika baada ya wananchi kuvua katika kata nane za Jimbo la Kigoma Kusini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa

Nashon Bidyanguze, Mbunge wa Uvinza, Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini tutatengeneza miundombinu? Narejea tena kama tulivyokwisha kujibu katika jibu letu la msingi, tunayo programu ambayo ni katika bajeti yetu ya mwaka 2022/2023. Lakini kwa upande wa Kigoma Kusini tunalo Shirika Lisilokuwa na Kiserikali *(NGO)* linaitwa TUUNGANE, linafanya kazi kubwa na nzuri sana ikishirikiana na Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Kigoma na Rukwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuliunga mkono shirika hili kwa kuwa lina programu bora na nzuri sana itakayoweza kuwasaidia wananchi wa kule Kigoma. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Gwajima swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Kawe, Jijini Dar es Salaam nusu ya kata yake ziko mwambao wa Bahari ya Hindi kwa maana ya Kata ya Msasani, Kata ya Kawe, Kata ya Kunduchi, Kata ya Mbweni na Kata ya Bunju.

Ni lini sasa Mheshimiwa Waziri utakuja kukaa na wavuvi wetu wa Jimbo la Kawe ili kutatua kero zao ndogo ndogo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Askofu Gwajima, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Bunge niko tayari kwenda kwa ajili ya kuweza kuzungumza na wavuvi wa Kawe na tunao Mradi wa *SWIOFISH* ambao yeye na mimi tutakwenda na wataalam wetu kwenda kuzungumza nao wavuvi wetu na kuona fursa zinazoweza kupatikana za kuweza kuwasaidia na kusaidia Taifa letu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Bwawa la Kalemawe lililoko Jimbo la Same Mashariki ni bwawa ambalo lilikuwa limepangwa na *UNCDF* kuwa kituo kikubwa cha kufundishia wananchi wa *East Africa Community* na *SADC* kufuga samaki wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa bwawa lile limejaa matope, kwa hiyo hawawezi kuweka *cages*. Serikali ina mpango gani kusaidia ili ule mradi usije ukapotea? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaboyoka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimelichukua jambo hilo na sisi tutashirikiana na wenzetu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuona uwezekano wa kufanya *decantation* kwa maana ya kuondoa matope yale ili tuweze kuwanufaisha wananchi wa pale Same kupitia miradi ya samaki. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; ongezeko la maji katika Ziwa Tanganyika limeharibu miundombinu ya soko la samaki la eneo la Kibirizi. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kurudisha miundombinu hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2022/2023 kwa maombi ya Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda tayari Serikali tumeshatenga soko, tunaenda kujenga soko zuri litakaloweza kuwasaidia Wavuvi wa Kigoma. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nyoka, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante; je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya jengo la kufanyia biashara ya samaki na dagaa katika Kata ya Mbambabay, Wilayani Nyasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Nyoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshajenga soko katika mwambao wa Ziwa Nyasa eneo hili alilolitaja na tuko katika

hatua za mwisho ya soko hili na miundombinu yake kuikamilisha, na tayari Serikali na wao Waheshimiwa Wabunge wa Nyasa, akiwemo Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, kwa lengo la kuweza kwenda kufungua soko lile na kuweza kuwawezesha wavuvi wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali la msingi alisema kwamba katika mwaka huu wa fedha mtakopesha boti 300. Sasa nilitaka tu nijue kwa kuzingatia kwamba Jimbo la Kawe nusu yake ni wavuvi, lakini kwa kuzingatia kwamba tuliahidiwa boti na Mbunge wetu bado hatujapa.

Je, katika mwaka huu wa fedha tutapata boti ngapi katika hizo 300?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Halima, wewe mwenyewe Mbunge au na wewe uko sehemu ya hiyo ahadi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tayari ninalo ombi la Mheshimiwa Askofu Gwajima, Mbunge wa Kawe ya kwenda kufanya naye ziara ya kuzungumza na wavuvi wa Kawe. Na nimeshamhakikishia tunao mradi maalum wa *SWIOFISH* wa kuhakikisha kwamba tunawawezesha wavuvi wa Kanda ya Pwani; na miongoni mwa watakavyovipata ni hizi boti, Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, itakwenda kufanya kazi

hii na wavuvi wetu watainuka na kuongeza tija na kuongeza pato la Taifa letu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa nimeshuhudia mara nyingi wavuvi wakiwa wanafariki kutokana na kupinduka kwenye ziwa kwa mawimbi yale makubwa yaliyopo; na inachukua muda mrefu sana kupata boti kutoka Mbambabay kwenda katika sehemu nyingine za mbali.

Je, ni lini Serikali itawezesha eneo la Ng'ombo lenye wavuvi wengi kupata boti ambalo litawasaidia pia katika uokoaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hili ni ombi juu ya kuweza kupata boti ya doria kwa lengo la kuwanusuru wavuvi wanapopata ajali. Nimelichukua ombi hili, nitakwenda kulifanyia kazi na kuhakikisha kwamba wavuvi wale na wenyewe wa pale Nyasa wanapata boti itakayowasaidia katika lengo hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika Ziwa Nyasa kuna samaki na dagaa ambao ni maarufu sana na ni wazuri sana kwa chakula; ni lini Serikali itatangaza aina hizo za samaki ikiwemo mbasa, ndelele pamoja na usipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunao Samaki wazuri aliyowataja mbasa na wengine kama vitui, kutoka katika Ziwa Nyasa. Na anataka kujua lini tutafanya kuwatangaza na kuwapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, jambo hili nimelichukua na miongoni mwa maeneo ambayo tutawapa kipaumbele ni eneo la Ziwa Nyasa ili mazao yanayotoka pale yaweze kuwa ni sehemu ya kipaumbele chetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi ama wavuvi wa Bwawa la Chimendeli ni wavuvi ambao wamesahaulika na wamekuwa wakifanya uvuvi wao kwa zana duni na kutokupata tija ya mazao ya uvuvi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wavuvi hawa wa Chimendeli pamoja na Bwawa la Mtera ili waweze kupata vifaa bora na waweze kuvua uvuvi wenye tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Majala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema katika jibu la msingi, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ni Serikali sikivu. Moja ya kipaumbele chake ni kuwainua wavuvi, na kwa hivyo tunao mpango na programu na tumetenga bajeti. Mheshimiwa Kunti na Wabunge wengine tuandae wavuvi wetu, mara tu baada ya kuwa tayari programu hii waweze kukopa wakiwemo wavuvi kutoka Mtera waweze kunufaika na rasilimali zetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanzisha soko la kimataifa ili kuuza samaki wanaovuliwa hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, tunayo masoko ya kimataifa, lakini nachukua ombi hili na maelekezo haya ya ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Maryam Mwinyi ya kwamba tuongeze masoko mengine ya

kimataifa. Kwa hiyo katika mipango yetu na mikakati yetu tutatekeleza ushauri huu wa Mheshimiwa Mbunge, Maryam Mwinyi, wa kutanua zaidi masoko ya Kimataifa katika nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kuna pesa ambazo zilikuwa zimeletwa Mwibara kwa ajili ya ujenzi wa josho kwenye Kijiji cha Chungurubila, lakini zikarejeshwa Serikalini. Je, ni lini pesa hizo zitarudishwa tena Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mfumo wa upelekaji wa pesa za majosho kama alivyosema, kwenye mfumo wa mwaka 2021/2022 yako matatizo na changamoto tulizoziona, tumeondoa mfumo ule na sasa tunakwenda na mfumo mpya ambapo pesa zile zitakwenda moja kwa moja katika Halmashauri ya Vijiji na mtasisimamia Waheshimiwa Wabunge na Mamlaka za Mikoa na Wilaya kuweza kuona urahisi pasipo kuwa na mgogoro wowote. Kwa kuwa katika mwaka uliyokwisha tuliona ni kweli kwamba pesa nyingi zilishindwa kutumika katika Halmashauri yetu ipasavyo; na kwa hivyo Mheshimiwa Kajege na Wabunge wengine jueni tu kwamba majosho ya safari hii mtakwenda kuyasimamia ninyi wenyewe ambapo yapo zaidi ya majosho 400 yaliyotengwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Katika Mji wetu wa Iringa tuna Mto Ruaha unakatisha pale na tuna vijana wanafuga samaki kwa njia ambazo siyo za kisasa sana.

Je, Serikali inaweza kutusaidia ili kuwapa mafunzo labda na kutujengea kizimba ambacho kinaweza kuwasaidia ili wafuge kisasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimechukua ombi lake hili na kwa kuwa tayari katika programu na bajeti yetu ya mwaka 2022/2023 tunazo halmashauri zitakazokwenda kupelekewa mashamba darasa. Basi Wilaya ya Iringa inaweza kwenda kuwa ni miongoni mwa watakaonufaika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; kwa kuwa soko la samaki la Kimataifa la Kasanga lililojengwa na Serikali kwa bahati mbaya sana lilikumbwa na mafuriko.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba soko hili linajengwa ili likidhi haja iliyokuwa imekusudiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephat Kandege, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli soko letu la Kasanga lilimezwa na maji, lakini tunayo programu ya kuweza kutenga bajeti tayari na kwa hivyo kuweza kujenga miundombinu upya ili kuweza kuwasaidia wavuvi wetu wa pale Kasanga na mwambao wa Ziwa Tanganyika ili kusudi waweze kuendelea kutumia fursa ya rasilimali samaki na dagaa wa Ziwa Tanganyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Tabasam, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Sengerema unafahamu kwamba ni eneo ambalo lina eneo kubwa la wavuvi. Je, katika hizi mashine 300 za boti, Sengerema tumo katika orodha hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamis Tabasam, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye fursa hii ya boti zaidi ya 300 za kuwezesha wavuvi wadogo wadogo kukopa, Sengerema na wenyewe wamo. Kwa hivyo Mheshimiwa ajitahidi katika kuhakikisha kwamba anawapanga wavuvi wake wawe tayari, fursa itakapokuwa wazi waweze kuitumia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wetu wamekuwa wakitumia zana duni sana, hasa wa Jimbo langu la Mtwara Vijijini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanatoa zana bora kwa wavuvi wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 imetengwa pesa ya kununua boti zaidi ya 300 kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo, na boti hizi zitakuwa na vifaa vya kisasa. Kwa hiyo ni matumaini yangu kwa kushirikiana Benki ya Kilimo, tuwaandae wavuvi wetu ili waweze kuweza kupata hizi pesa zitakazowaondoa katika matumizi ya zana duni na kuwafanya waweze kutumia zana za kisasa na kupata rasilimali za kutosha. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani mtakubaliana nami maswali yaliyojibiwa ni mengi sana na Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa sasa aulize swali lake.

Na. 487

**Hitaji la ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa Manda na Mkiu – Liganga hadi Madara kwa kiwango cha lami**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda na Mkiu – Liganga hadi Madaba kwa Kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Itoni – Ludewa - Manda yenye urefu wa kilometa 211 na barabara Mkiu – Liganga - Madaba yenye urefu wa kilometa 112 imekamilika. Serikali inaendelea na kazi za ujenzi kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya barabara ya Lusitu - Mawengi yenye urefu wa kilometa 50. Ujenzi wa barabara sehemu ya Itoni - Lusitu kilometa 50 kwa kiwango cha zege umeanza. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi kwa sehemu zilizobaki. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kipande cha barabara kutoka Mawengi mpaka Manda ni eneo ambalo lina Mlima Kimelembe, mlima huu umekuwa ukisababisha ajali nyingi kutokea, wananchi wengi wamepoteza maisha na kupata ulemavu, lakini vilevile imekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa uwekezaji wa usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka Nkomang'ombe. Na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri amekwenda kule mara nyingi.

Sasa je, Serikali haioni haja ya kushughulika na huu Mlima Kimelembe ili kuepusha ajali kwa wananchi, lakini vilevile kurahisisha hawa wawekezaji wa makaa ya mawe waweze kusafirisha makaa ya mawe?

Mheshimiwa Spika, na swali la pili, katika ujenzi wa kipande kile cha Lusitu - Mawengi kuna wananchi wanne wa Kata ya Mlangali hawajalipwa fidia na wananchi kama 72 wa kata ya Mawengi. Je ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maombi ya kufanya ujenzi kwa maana ya kurekebisha Mlima Kimelembe yaliletwa na Mheshimiwa Mbunge, lakini pia Kamati ya Miundombinu ilitembelea barabara hii tarehe 11 Juni. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ludewa kwamba kwa kuwa barabara hii ilishafanyiwa usanifu kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, tayari Meneja wa Mkoa wa Njombe alipewa maagizo ya kufanya tathmini ya gharama ya kutengeneza ule mlima, kuuchimba kwa kiwango kilekile

ambacho tutakijenga ili tusirudie mara mbili na tayari Makao Makuu *TANROADS* wanafanyia tathmini ili kuweza kuujenga huo mlima kwa kiwango cha lami, ama cha zege, ama cha mawe kilomita tano.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu suala la pili la fidia; wako wananchi ambao kweli waliwekewa alama za kijani japo bado hawajaguswa hasa eneo la Mlangali, wananchi hawa tayari Serikali inatafuta fedha ili tutakapohitaji maeneo yao basi tuweze kuwafidia na waweze kupisha kwa sababu wapo kwenye eneo la hifadhi ya barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Naomba kujua mpango wa Serikali wa kuunganisha Jimbo la Ukonga na Jimbo la Temeke kupitia eneo la Msongola mpaka Mbande la kilometa 4.95. Kwa sababu tayari kwenye bajeti hii imetengwa kilomita mbili na tuliomba kutengewa kilometa zote 4.95? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuunganisha hili Jimbo pamoja na Wilaya ya Temeke kwa kiwango cha lami na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba mpango huo upo kwa kusaidiana na wenzetu wa TAMISEMI tutahakikisha kwamba barabara hiyo inaunganishwa ili

kurahisisha usafiri kati ya Ukonga kwa maana ya Ilala na Temeke kwenda Msongola. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana; kutokana na umuhimu wa kiuchumi mkubwa kwa Mikoa ya Mbeya, Songwe na nchi jirani ya Malawi; je, ni lini barabara ya Mbalizi - Shigamba - Isongole itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi - Shigamba kwenda Isongole ambako ni kwenda Malawi ni barabara muhimu sana kwa uchumi na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba mwaka huu wa fedha barabara hii imetengewa fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi kwa kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Barabara ya Katesh - Hydom kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 imetengewa milioni 280 kwa ajili ya usanifu wa kina. Je, Serikali iko tayari kujenga eneo la Mlima Chavda

ambao mara nyingi imekuwa ikisababisha ajali kwa kutumia fedha za matengenezo kwa mfumo wa kusanifu na kujenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baraba ya Katesh - Hydom ni *link* ya barabara kuu ya Karatu - Mbulu kwenda Sibiti. Kwa hiyo taratibu zote ambazo zitafanyika katika hiyo barabara, hii barabara pia ni sehemu ya hiyo barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. barabara inayotoka Masungwe Mkoa wa Geita na Mwabomba katika Mkoa wa Shinyanga ina hali mbaya sana na inahatarisha maisha ya wananchi wanaofanya shughuli zao za uchimbaji katika Mgodi wa Mwabomba.

Ni lini sasa Serikali itaanza kuijenga barabara hiyo hasa mpaka huo ambao ni daraja linalounganisha Mwabomba na Masumbwe ili wananchi wasiendelee kupata shida katika shughuli zao za uchimbaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu

swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja yako maeneo ambayo yalikuwa ni barabara ya *TANROADS* na mengine yalikuwa ya *TARURA,* lakini sasa inahudumiwa na *TANROADS*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha imetengwa kwa ajili ya kuanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii sasa itapitika kwa kipindi chote cha mwaka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene - Kaisho hadi Murongo ni barabara ya kiuchumi; je, ni lini Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge sijaisikia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mheshimiwa Naibu Waziri hajasijikia jina la hiyo barabara.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene - Kaisho hadi Murongo; ni lini Serikali itajenga kwa kiwango lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene kwenda Murongo kuna barabara mbili ambayo moja inapita kwenda Murongo, lakini nyingine inapita Umugakalongo kwenda Murongo. Barabara zote hizi moja tayari imeshatangazwa na nyingine tuko kwenye kufanya *evaluation* kuanza ujenzi wa barabara na hiyo barabara ya Murongo - Bugene tutaanza kuijenga kuanzia upande wa Murongo mpakani na Uganda, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kuweza kuniona.

Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya, Tabora na Singida ni moja kati ya barabara muhimu sana kiuchumi lakini pia imeahidiwa mara kadhaa kuweza kujengwa lakini mpaka sasa hivi haijaanza kujengwa. Je, ni lini sasa barabara kuanzia Makongorosi kuelekea Mkiu itaanza kujengwa kipande cha kuanzia Makongorosi ndani ya Wilaya ya Chunya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimwa Spika, napenda kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Makongorosi kwenda Mkiu - Singida ni barabara kuu na barabara hii tayari imeshaanza kujengwa kuanza kwa kutoka Mbeya hadi Makongorosi, lakini sasa hivi imeshatangazwa nadhani Mkandarasi atakuwa yupo *site* upande wa Mkiu kuelekea Itigi kwenda Rungwa. Serikali sasa inafanya mpango wa kutafuta fedha ili ikiwezekana tuweze kutangaza zaidi ya *lot* moja na kama tutapata basi tutaangalia uwezekano wa kuanza upande wa Makongorosi ili tukutane katikati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii ambayo umenipa.

Jimbo la Lupembe na kule Mkoa wa Morogoro ni *corridor* muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu; na kuna ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa barabara ya Kibena - Madeke. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edwin Swalle, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibena – Madeke - Mlimba hadi Ifakara tumeshaanza kuijenga kutokea Morogoro; na mwaka huu tumetenga kilometa 50 kwenye Jimbo la Mlimba ambapo nadhani tutaanza.

Kwa upande wa barabara aliyoitaja kuanzia Kibena kwenda Madeke barabara hii imeshafanyiwa usanifu na wenzetu wa *African Development Bank* wamekubali kufanya review ya usanifu na tumeshapeleka mapendekezo tunasubiri *no objection* ili waweze ku-*review* usanifu na kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu umuhimu wa kuwa *round about* katika eneo la Ndorobo ili kuepusha ajali katika barabara inayotoka Tabora kwenda Kigoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *round about* ambayo anaitaja ipo Mjini Urambo na Mheshimiwa Mbunge aliipigia kelele kwa sababu eneo lile halina *keep left* na lilikuwa linasababisha ajali. Mwaka huu nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumeingiza kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji na tayari tunaamini kwamba mwaka ujao wa fedha kwa sababu ni eneo muhimu kwa ajili ya usalama wa wana Urambo, *keep left* hiyo inakwenda kwenye hiyo barabara kuu ya Tabora - Urambo, Uvinza - Kigoma. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Aboud, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimwa Spika, ahsante; je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Likuyufusi kwenda Mkenda pamoja na Daraja la Mitomoni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khadija, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Likuyufusi - Mkenda ni barabara kuu ambayo inaunganisha nchi ya Tanzania na Msumbiji kupitia Jimbo la Peramiho. Lakini pia katika hii barabara kuna Daraja la Mitomoni, mwaka huu nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho kwamba tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza na ujenzi wa kilometa zisizopungua 50 pamoja na Daraja la Mitomoni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimwa Spika, ahsante sana; barabara ya Katumba – Songwe – Kasumulu – Ngana - Ileje ni barabara muhimu sana siyo tu kwa ajili ya ulinzi bali pia kwa uchumi wa Kusini mwa Tanzania.

Je, ni lini Serikali itaanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimwa Spika, ahsante, napenda kujibu

swali la Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara aliyoitaja ni muhimu kwa uchumi, lakini pia ni barabara ya ulinzi, lakini pia ndiyo barabara ambayo inasaidia kupitisha makaa ya mawe kutoka Mgodi wa *Kiwira Coal Mine* na kwa sababu hiyo, Serikali inakamilisha Usanifu wa Kina na katika mwaka wa fedha unaokuja fedha imetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Isongole – Malangali – Ikinga – Ngana - Kasumulu hadi Katumbasongwe kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Livingstone Lusinde swali la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Naomba majibu ya Serikali kuhusu barabara ya kutoka Dodoma Mjini - *Ntyuka Junction- Mvumi Mission*; ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lusinde, Mbunge wa Mvumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii barabara ni muhimu na Mheshimiwa Mbunge amekuja mara kadhaa na tumemhakikishia kwamba barabara hii ipo kwenye utaratibu wa kuijenga kwa mwaka ujao, lakini ombi lake kubwa ilikuwa ni kwamba tuanze Mvumi suala ambalo nadhani

Mheshimiwa Waziri tulimuahidi kwamba tutafanya hivyo kama alivyoomba. Kwa hiyo, mwaka ujao wa fedha tunaanza na kuijenga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Barabara ya Korandoto kwenda Mbunze hadi Mwangongo yenye kilometa 63 ni barabara iliyokuwepo kwenye mpango wa utekelezaji wa mwaka 2021/2022 ilikuwa imetengewa shilingi bilioni mbili ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami lakini mpaka sasa haijaanza kujengwa.

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa katika kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii pia ni kati ya barabara kuu ambazo bado hazijajengwa kwa kiwango cha lami na ni kipaumbele kwa Wizara na Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti pia ya mwaka ambayo tunakwenda kuitekeleza imetengewa fedha na tunaamini

kwamba barabara hii pia itajengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spik,a barabara ya Singida – Simiyu kilometa 42 zinafika Makao Makuu ya Wilaya, wakati tunasubiri huruma ya *EPS+F* barabara hii ni muhimu ikafanyiwa ukarabati.

Je, Waziri anasemaje kwa sababu kwa sasa barabara imejaa mawe kiasi kwamba watu wanapasua matairi na wanashindwa kupita? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Isack Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara uliyosema ya Singida kwenda Simiyu, nataka tu nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo tutaikarabati ili iweze kupitika kwa kiwango cha changarawe, na kwa mazingira aliyotoa naomba nimuagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Singida kuhakikisha kwamba anakwenda kutembelea hiyo barabara na kuhakikisha kwamba inaanza kufanyiwa ukarabati haraka iwezekanavyo kipindi hiki cha kiangazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; kwa kuwa mchakato wa ujenzi wa kilometa 25 kutoka Mbulu kwenda Garbabi uko tayari na mkandarasi alipatikana.

Je, ni lini Serikali sasa Mkandarasi ataanza kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo ya kilometa 25 kutoka Mbulu Mjini kwenda Garbabi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara kama alivyosema mkandarasi alishapatikana na ni taratibu tu za manunuzi zinakamilishwa ili mkandarasi huyo aanze kazi kujenga hizo kilometa ambazo zimeshatangazwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kwa swali la nyongeza. Barabara ya kuanzia Gairo – Ngiloli – Chakwale - Iyogwe mpaka kuunganisha na Kilindi, Mkoa wa Tanga; je, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ni muhimu sana? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja kutoka Wilaya ya Gairo kwenda Kilindi ni barabara ya Changarawe, lakini kwa sasa kitu ambacho tunakifanya ni kuhakikisha kwamba kwanza tunajenga madaraja mawili ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa sana. Daraja la Chakwale na Nguyami ni madaraja ambayo kwa sasa tunayafanyia usanifu ili kuyajenga yaweze kupitika, lakini pia kuimarisha barabara kwa kiwango cha changarawe. Lakini baada ya hapo ndiyo tutaanza sasa kukamilisha usanifu kwa ajili ya maandalizi kwa ujenzi wa lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa nchi yetu sasa hivi inashuhudia ongezeko kubwa la watalii kutokana na kazi nzuri iliyofanywa kwenye *Royal Tour,* lakini vivutio vingi havifikiki kwa urahisi wakati wa masika.

Je, Serikali ipo tayari wakati wa *Mid-year Review* kuja na mpango kupitia *EPC+Finance* kwa barabara kwa mfano inatoka Kisarawe - Manerumango, - Vikumbulu - Mloka na Kibiti – Mloka kwa ajili ya kuhakikisha mbuga yetu ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere inafikika kwa urahisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu

swali la nyongeza la Mheshimiwa Subira Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanyakazi kwa pamoja, wakati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anafanyakazi kubwa ya kuifungua nchi na kuitangaza na sisi kila sekta ikiwepo ya miundombinu ambayo tunajua, tunafanya *facilitation* ya hao watalii mbalimbali kufika sehemu za vivutio.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tumeliona na mpango aliosema moja ya barabara ambazo zinakwenda huko za Manerumango lakini pia kupitia Wilaya ya Rufiji zipo kwenye huo mpango na hata hii ya *Serengeti bypass* tayari imeingizwa kwenye huo mpango ikiwa tu ni jitihada za Wizara, lakini kuhakikisha kwamba watalii wanafika maeneo yenye vivutio bila shida, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameshajibu maswali mengi sana, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla ya suala hili la maswali nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI atoe ufafanuzi kidogo kuhusu wanafunzi wa kidato cha nne wanaotaka kubadili kutoka vyuo kuelekea kwenye shule za kidato cha tano na cha sita. Hebu toa ufafanuzi hao wanafanya nini ili waweze kuhama. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ufafanuzi na nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa *concern* ambazo wamekuwa wakizionesha juu ya mahitaji ya wazazi, walezi na watoto wetu ambao wanahitaji kubadilisha shule kama ni *form five* kwenda shule nyingine, lakini kwa wale ambao

wamepangiwa vyuo kubadilisha vyuo au kutoka kwenye vyuo kwenda *form five*.

Mheshimiwa Spika, baada ya watoto wetu kuripoti mashuleni tumetoa wiki mbili; kwanza wafike kwenye maeneo ambayo wamepangiwa halafu baada ya hapo tutaweza kujua wale watoto ambao wanahitaji kuhamishwa tupate orodha ambayo ni kamilifu ili tuweze kuiratibu na kuwapangia kwa mujibu wa nafasi ambazo zinakuwa zimepatikana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, baada ya wiki mbili tunaomba muendelee kuwa na subira na tumefanya jambo hili kwa sababu ni jambo ambalo linafanyika kila mwaka. Kwanza watoto waripoti maeneo ambayo wamepangiwa/wamechagua na sisi tukaratibu maeneo ambayo wamepangiwa; halafu wiki mbili zikiwa zimekamilika tutakuwa tumeshapata orodha kamili ya maombi ya walezi na watoto wetu na kuweza kuratibu kulingana na nafasi ambazo zinakuwa zimepatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikushukuru kwa nafasi ya kuweza kutoa ufafanuzi huu, niendelee kuwaomba wazazi, walezi na watoto wetu waendelee kutupa ushirikiano wakati Serikali tunaratibu na kukamilisha zoezi hili. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nilete matangazo niliyonayo hapa mbele, tangazo la wageni.

Tunao wageni hapa Bungeni na tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika; wapo wageni wanne Wabunge ambao ni Mheshimiwa Paul Kabuswe ambaye ni Waziri wa

Madini na Maendeleo ya Migodi, Zambia, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Sakwiba Musiwa ambaye ni Katibu Mkuu, Wizara ya Madini na Maendeleo ya Migodi, Zambia, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Pamela Nakombe ambaye ni Afisa Mipango Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mhandisi Elite Leonard Mhone ambaye ni Mhandisi wa Migodi Mwandamizi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wageni hawa wamekuja kutembelea Wizara ya Madini kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na viongozi wa Wizara hii ikiwa ni pamoja na kujifunza namna ya kuendesha sekta ya madini hasa wachimbaji wadogo wa madini. Karibuni sana wageni wetu kutoka Zambia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika Jukwaa la Spika, pia wapo wageni 47 wa Bunge ambao ni viongozi watano na wanakwaya 42 kutoka Chuo Cha Utumishi wa Umma wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo - Mipango, Fedha na Utawala. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge; karibuni sana wageni wetu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa wameongozana na Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala, Dkt. Ernest Mabonesho, karibu sana na ahsanteni sana pia kwa huduma nzuri muliyoitoa jana, asanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia Jukwaa la Spika, yupo Bi. Jacqueline Kawishe ambaye ni Mkurugenzi wa *Baron Group Dar es Salaam,* hawa wanatengeneza viatu. Haya, nafikiri hawajaingia, lakini wameshatangazwa kwa hiyo, yuko wapi? Amesimama wapi? Lakini pia huyu ameongozana na Bi. Nasikiwa Beria, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wako hapa ndani. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana wageni wetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao walimu wawili na wanafunzi 44 wa Shule ya Awali na Msingi ya *Zion Mission* kutoka Ntyuka, Jijini Dodoma, karibuni sana watoto wetu na walimu wenu, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni saba kutoka Asasi ya Vijana Afrika ambayo inaitwa *Africa Youth Transformation* wakiongozwa na Ndugu Arafat Lesheve, huyu ni Mratibu Mkuu wa Tuzo za Vijana Chipukizi Tanzania chini ya Asasi ya Vijana ya *Africa Youth Transformation* na mwakilishi wa vijana kitaifa katika Baraza la Vijana la Jumuiya ya Madola, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao. Sasa kabla sijasimama hapa nimemsikia Mheshimiwa Mpina akisema Mwongozo kwa maana ya kwamba kuna jambo limetokea mapema hapa leo asubuhi na anataka kujua kama linaruhusiwa au haliruhusiwi. Mheshimiwa Mpina.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kuomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 70(1) na (2).

**SPIKA:** Kanuni ya 70 Mwongozo Mheshimiwa Mpina? Kanuni ya 70 inasemaje?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kutosema uongo Bungeni.

**SPIKA:** Sasa hiyo sio kanuni inayohusika. Anayezungumza kusema uongo unayetaka kumzuwia sasa hivi ni nani? Unayetaka kumzuia yaani kusema uwongo ni nani? Waziri kasema uongo? Kwa sababu, lazima liwe, kwa hiyo, nielezee ili nielewe hoja yako, Mwongozo kuhusu nini?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ninalotaka kulizungumzia lililosemwa uongo hapa Bungeni limetokea tarehe 24/6/2022 na tarehe 18/05/2022...

**SPIKA:** Basi kaa chini.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kanuni zetu hizi kwa sababu, mimi haiyumkiniki kwamba Spika atakuwa anakumbukumbu ya hayo mambo kichwani ili sasa niweze kutoa hiyo nafasi ya Mwongozo. Mwongozo...

Kwanza ngoja nisimame maana leo ni siku muhimu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ukisimama hapa Bungeni ukasema Mwongozo wa Spika, unaongozwa na Kanuni ya 76 ambayo inakupa nafasi ya wewe kusema Mwongozo wa Spika ili unaomba Spika atoe ufafanuzi juu ya jambo lililotokea mapema Bungeni kama linaruhusiwa au haliruhusiwi. Kwa hiyo, ukisema tu Mwongozo wa Spika tunaenda kwenye Kanuni ya 76, sio iliyomuongoza Mheshimiwa Mpina.

Sasa nilipomuuliza jambo gani, ameenda kwenye kanuni anasema Kanuni ya 70 na inazungumzia Kuhusu Kutokusema Uongo.

Waheshimiwa Wabunge, ukiisoma hii kanuni kwa sababu ni ndefu na nimesema leo ni siku maalum, sitapata muda wa kufafanua kwa kirefu, lakini isomeni Kanuni ya 70 ni mazingira gani unaweza kusimama ili uitumie kanuni hii. Kwa

hiyo, tusome mazingira inayosema hapo ambayo hakuna mahali ambapo naweza kutoa sasa hiyo nafasi kwa sasa hapa kwa kupitia Kanuni ya 76, ili nielekee sasa kwenye 70.

Waheshimiwa Wabunge utaratibu uko vizuri kabisa. Kwa hivyo, tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Mkutano wa Saba wa Bunge, sasa zimekamilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikia Katibu wa Bunge akitueleza kwamba ratiba yetu imekamilika, na sasa nimuite tena kwa ajili ya ratiba inayofuata.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja ya Kuahirisha Bunge, nimuite Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ili aje asome hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuhitimisha shughuli zote za Mkutano wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa buheri wa afya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vema mijadala ya Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili; Wabunge, mtakubaliana nami kwamba katika kipindi hiki kifupi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini toka ashike wadhifa wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha ukomavu, uhodari na umakini mkubwa katika kuliongoza Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwapongeze sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini pamoja na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuonesha umahiri na weledi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kuhakikisha shughuli zote za mkutano huu zinakamilika kama zilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa hoja za bajeti za Wizara zao, kutoa ufafanuzi wa kina katika kujibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mijadala ya hoja hizo. Ni matumaini yangu kwamba baada ya kuhitimishwa kwa shughuli za mkutano huu, sasa watakwenda kusimamia ipasavyo sekta zao ili kuhakikisha bajeti zilizowasilishwa zinagusa maeneo ya msingi na maslahi mapana ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitotambua ushiriki mzuri wa michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzagu wakati wote wa Mkutano huu tangu ulipoanza tarehe 5 Aprili 2022. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwani michango na ushiriki wenu umekuwa chachu katika kufanikisha shughuli za Mkutano wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan katika kutekeleza kikamilifu wajibu wetu wa Kikatiba wa kupitia, kujadili na kupitisha Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kwa upande wake itazingatia maoni na ushauri wenu kwa ajili ya kulinda maslahi mapana ya Watanzania. Aidha, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa katika kipindi hiki tunaporejea majimboni kwetu tukawe mabalozi wazuri kwa wananchi tunaowatumikia kuhusu mambo mengi muhimu yaliyojiri katika kipindi chote cha Mkutano huu hususan mipango na mwelekeo wa Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, salamu za pole; tarehe 24 Aprili, 2022 wakati tukiendelea na shughuli za Mkutano wa Saba wa Bunge lako tukufu, tulipokea taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Irene Ndyamkama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha Mapinduzi kilichotokea katika Hospitali ya Tumbi iliyopo Kibaha, mkoani Pwani. Hivyo basi, nami kwa masikitiko makubwa naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kufuatia kuondokewa kwa mpendwa wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, pia tumeshuhudia kutokea kwa ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri zikihusisha pikipiki, magari, treni na kadhalika. Ajali hizo

zimesababisha vifo vya wapendwa wetu, uharibifu wa mali na pengine ulemavu. Kwa msingi huo, nitoe pole kwa Watanzania wenzangu waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata majeraha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo matukio ya ajali za vyombo vya usafiri na niwatakie afya njema na uponyaji wa haraka wale wote waliojeruhiwa na tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kupitia, kujadili na hatimaye kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Bunge lako tukufu pia lilipata fursa ya kupokea maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kutolewa majibu kutoka upande wa Serikali. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria, Maazimio ya Bunge na kupokea Kauli za Serikali katika kutolea ufafanuzi hoja kadhaa zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zilihitaji kupata kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Saba wa Bunge la Kumi na mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jumla ya maswali 487 ya msingi na mengine 2,115 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Halikadhalika, jumla ya maswali 19 ya papo kwa papo yaliulizwa na Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Miswada ya Sheria minne iliweza kujadiliwa na kupitishwa na Bunge lako tukufu. Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2022 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa mwaka 2022 ilisomwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, vilevile Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022 na Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali ulisomwa kwa hatua zake zote.

Mheshimiwa Spika, Maazimio; vilevile Bunge lako tukufu lilifanikiwa kujadili na kupitisha Maazimio matatu ya Bunge yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Azimio la kwanza ni Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani na kupewa tuzo ya juu ya Mjenzi Mahiri ya Babacar Ndiaye kufuatia mafanikio makubwa katika ujenzi wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio la pili ni Azimio la Bunge la kuipongeza timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa Miguu *(Serengeti Girls)* baada ya kufuzu michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika nchini India mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Azimio la tatu ni Azimio la Bunge la kuipongeza timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wenye Ulemavu *(Tembo Warriors)* kufuatia kufuzu kwao michuano ya kombe la dunia itakayofanyika mwaka huu nchini Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kauli za Serikali; kwa kuzingatia Kanuni ya 56 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020, Waheshimiwa Mawaziri walitoa kauli rasmi za Serikali Bungeni ikiwa ni ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja hizo zilihusu baadhi ya mambo yaliyotokea nchini na kugusa moja kwa moja maslahi ya wananchi. Kauli zilizotolewa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutoka Wizara ya Nishati; kupitia Mkutano huu Mheshimiwa Januari Yusuf Makamba, Mbunge, Waziri wa Nishati alitoa Kauli ya Serikali Bungeni kuhusu kupanda kwa bei za mafuta na hatua zinazochukuliwa kushughulikia suala hilo. Serikali pamoja na mambo mengine ilitoa mwenendo wa bei ya mafuta, mipango ya muda mfupi

na muda mrefu kukabiliana na changamoto hiyo pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa ikiwemo kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 ili kupunguza makali ya bei ya mafuta hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; vilevile Mheshimiwa Hamad Masauni, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa Kauli ya Serikali Bungeni kuhusu Watanzania walioko nje ya Nchi kurudi nchini kushiriki shughuli za ujenzi wa Taifa. Kauli hiyo, imezingatia hali nzuri ya kisiasa na kiusalama nchini pamoja na hatua za dhati zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kila Mtanzania, wakiwemo viongozi wa kisiasa waliopo ndani na nje ya nchi, wanashiriki katika shughuli za ujenzi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita; leo tunaelekea kuhitimisha shughuli za Mkutano wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili, aidha, kupitia Mkutano huu, pamoja na mambo mengine Bunge lako tukufu limefanikiwa kupitia, kujadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Bajeti tuliyoipitisha imeendelea kututhibitishia nia njema, uthubutu wa hali ya juu na azma ya kweli ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutelekeza mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwaletea watanzania maendeleo ya haraka sambamba na kuwakwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mengi yameelezwa na kufafanuliwa na Waheshimiwa Mawaziri wakati wakiwasilisha hoja za bajeti za sekta zao na wakati mwingine hata Waheshimiwa Wabunge wakati walipokuwa wakichangia hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri. Kwa lugha nyingine, kupitia hotuba hii ya kuhitimisha shughuli za Serikali zilizopangwa kwenye Mkutano wa Saba wa Bunge

la Kumi na Mbili, nisingependa kurudia kile kilichojadiliwa wakati wote wa Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, niruhusu nitumie fursa hii kugusia kwa uchache baadhi ya mambo ya msingi ambayo yataakisi taswira, dhamira, nia, uthubutu, maono na azma ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha kuwa Taifa letu linapiga hatua za haraka za maendeleo ndani ya kipindi kifupi. Miongoni mwa mambo hayo ni ujio wa filamu ya *Royal Tour,* ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 na kuwekwa saini kwa makubaliano ya Awali ya Utekelezaji wa Mradi wa Usindikaji Gesi Asilia *(LNG)*.

Mheshimiwa Spika, filamu ya *Royal Tour;* Bunge lako tukufu litakubaliana nami kwamba sekta ya utalii imeendelea kupata mafanikio makubwa hususan kufuatia uzinduzi wa filamu ya *Royal Tour* tarehe 28 Aprili, 2022 iliyozinduliwa Jijini Arusha. Filamu hiyo ya kihistoria imekuja katika kipindi muhimu ambacho sekta ya utalii na huduma ilikumbwa na athari za UVIKO-19. Hivyo, ujio wa filamu hiyo, umechangia kuimarisha shughuli za utalii na kusaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa sintofahamu nyingi kuhusu urithi na utalii uliopo Tanzania. Mheshimiwa Rais ameweza kuonesha uhalisia wa nchi yetu kuanzia vivutio vya biashara, utalii, madini na hata sanaa na utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matunda ya jitihada hizo za Mheshimiwa Rais yameanza kuonekana hususan kwenye sekta ya utalii na huduma ambapo watalii na wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali duniani wameanza kumiminika kuja hapa nchini. Mathalani, watu maarufu wakiwemo wachezaji wa mpira wa miguu kutoka ligi kuu mashuhuri Barani Ulaya na ligi ya mpira wa kikapu nchini Marekani wametembelea katika mbuga zetu katika kipindi hicho. Kadhalika Wakala wa Utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii yakiwemo Marekani, Israel, Ufaransa na Lithuania

wamehamasika kuja nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuitangaza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, mwezi Aprili, 2022 Serikali iliingia makubaliano na Jiji la Dallas lililopo nchini Marekani kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya utalii, biashara na uwekezaji. Hatua hiyo, inalenga kufungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, mwezi Aprili, 2022 Serikali iliingia makubaliano na Jiji la Dallas lililopo nchini Marekani kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya utalii, biashara na uwekezaji. Hatua hiyo, inalenga kufungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali ya utalii nchini ili kufikia lengo la kuvutia watalii milioni tano kwa mwaka sambamba na mapato ya Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025. Kuongezeka kwa idadi ya wageni wanaotembelea Tanzania, kutaimarisha sekta ya utalii na huduma nchini na hivyo kutengeneza fursa nyingi zaidi za ajira, kuwakwamua wananchi kiuchumi na kujenga uchumi imara na shindani.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miradi ya maji miji 28; itakumbukwa kuwa tangu akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa alijipambanua na mpango maarufu wa kumtua ndoo mama kichwani. Dhamira hiyo ya Mheshimiwa Rais imeendelea kujidhihirisha kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 uliozinduliwa tarehe 6 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo wenye thamani ya dola za Marekani milioni 500 utachangia kwa

kiwango kikubwa katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye miji iliyobainishwa ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mradi huo wa maji ambao ni mkubwa zaidi kuwahi kutokea nchini kwa wakati mmoja, utakapokamilika utahakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi wapatao milioni sita.

Mheshimiwa Spika, sambamba na upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, miradi hiyo pia itakuwa chachu kwenye kuvutia uwekezaji hususan wa viwanda. Serikali kwa upande wake, itahakikisha kuwa ujenzi wa miradi ya maji kwenye miji 28 unafungua fursa nyingine za kiuchumi zikiwemo ajira kwa wananchi wetu hasa kwenye maeneo ambayo miradi hiyo itatekelezwa. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuwasihi Watanzania wenzangu kuchangamkia fursa zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, niwasihi viongozi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushirikiane katika kuimarisha usimamizi wa miradi hii pamoja na kuhakikisha kwamba wakandarasi wanakamilisha miradi hiyo kwa wakati ili miradi hiyo iweze kutoa huduma iliyotarajiwa kwa wananchi wetu. Lakini vilevile niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa vinara katika kuwahamasisha wananchi kutunza mazingira na kuacha kufanya shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji kwani uhifadhi wa mazingira ndiyo msingi wa uendelevu wa upatikanaji wa majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Usindikaji Gesi Asilia *(LNG);* sote tumekuwa miongoni mwa mashuhuda wa kusuasua kwa muda mrefu kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa uchakataji wa Gesi Asilia *(LNG)*. Kwa msingi huo, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikiwa kutegua kile kitendawili cha muda mrefu cha lini ungekuwa

utekelezaji wa mradi wa uchakataji wa gesi asilia uliosimama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, tarehe 11 Juni tulishuhudia kuingiwa kwa makubaliano ya awali ya Mkataba wa nchi hodhi na kampuni za Kimataifa za utafutaji mafuta kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *LNG*.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais inatimia nitumie fursa hii kutoa wito kwa viongozi na watendaji wa sekta husika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi wa *LNG* unaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa Taifa letu ikiwa ni pamoja na kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na mauzo ya gesi, kuzalisha ajira za muda mfupi na za kudumu na kuimarisha mapato na uchumi wa Watanzania kupitia mauzo ya bidhaa na huduma mbalimbali wakati wa utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake itaendelea kuhakikisha kuwa inavutia uwekezaji unaokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 30 kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Vilevile naielekeza Wizara ya Nishati kuhakikisha kuwa inatumia vema fursa ya uwepo wa Mradi wa *LNG* kuimarisha uzoefu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* katika shughuli za gesi pamoja na kuwezesha upatikanaji wa gesi asilia iliyochakatwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mji wa Serikali; itakumbukwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mheshimiwa Rais aliridhia takribani shilingi bilioni 600 zitumike kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo 25 ya Wizara na taasisi kwenye Mji wa Serikali uliopo Mtumba Jijini Dodoma. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba ujenzi huo unaendelea vizuri na hadi kufikia

tarehe 24 Juni, 2022 umefikia kati ya wastani wa asilimia 30 hadi asilimia 56. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuhimiza Wizara na taasisi kuhakikisha wanaimarisha usimamizi ili ujenzi ukamilike ndani ya muda uliopangwa. Nitoe rai pia kwenu Waheshimiwa Wabunge mnapoondoka hapa Bungeni mpate muda kidogo wa kutembelea na kuona kazi nzuri inayoendelea kwenye mji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; katika kuhakikisha dhamira nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa inayojiakisi kwenye Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 inafikiwa, Serikali imejipanga vema kuendelea kusimamia suala la uwajibikaji katika utumishi wa umma. Mikakati iliyopo katika kuimarisha uwajibikaji hususan kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo: -

Kwanza, kuongeza bajeti ya matumizi mengineyo katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutoka shilingi bilioni 57.44 hadi shilingi bilioni 79.09 ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya ofisi hizo. Sambamba na ongezeko hilo la bajeti katika mwaka wa fedha 2022/2023. Serikali pia imehuisha muundo wa Sekretarieti za Mikoa kwa kuboresha iliyokuwa Sehemu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa na kuwa Sehemu ya Menejimenti, Ufuatiliaji na Ukaguzi ili kuimarisha ufuatiliaji wa mapato, matumizi na utekelezaji wa miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

Pili, kuendelea kuwajengea uwezo Waheshimiwa Mameya, Wenyeviti wa Halmashauri na Miji, Madiwani, Mafisa Tarafa na Watendaji wa Kata kupitia Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo ni kuongeza uelewa wa majukumu yao kisheria, kuimarisha mahusiano yao na viongozi wa kisiasa na

kusimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao pamoja na ukusanyaji wa mapato;

Tatu, kupima utendaji wa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kwa kutumia viashiria muhimu hususan usimamizi wa mapato na makusanyo ya ndani, upelekaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo, usimamizi wa mikopo ya asilimia 10 ikiwa ni pamoja na marejesho yake, usimamizi wa miradi ya maendeleo na uzuiaji na utekelezaji wa hoja za ukaguzi zinazoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*.

Mheshimiwa Spika, masuala ya ufuatiliaji na tathmini; eneo lingine lenye lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji Serikalini ni tasnia ya ufuatiliaji na tathmini. Tasnia hii mtambuka inahitaji uwepo wa mifumo na miundo imara ambayo itawezesha kujenga msingi thabiti wa usimamizi wa utendaji kazi wa Serikali. Kwa kuzingatia hilo, Serikali inaendelea kujenga mifumo na miundo wezeshi katika eneo la ufuatiliaji na tathmini ili kuboresha utendaji kazi unaojali matokeo.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zinajumuisha kupitia upya miundo na majukumu ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika eneo la ufuatiliaji na tathmini ili kuziimarisha pamoja na kujenga uwezo wa watumishi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali imeanza maandalizi ya Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa kuzihusisha taasisi simamizi zinazohusika na ufuatiliaji na tathmini ili kuchambua maeneo wanayosimamia na kuhakikisha maeneo yote muhimu yanajumuishwa ikiwemo usimamizi wa mipango ya maendeleo na utendaji wa Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, tayari Serikali imekamilisha Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ambao utaanza kutumika mwezi Julai, 2022. Mfumo huo, pamoja na mambo mengine utasaidia Serikali kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuongeza tija na thamani ya matumizi ya fedha za umma kwenye miradi husika.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imehuisha Muundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Ofisi ya Waziri Mkuu hususan kwa upande wa Sera, Uratibu na Bunge ili kuimarisha jukumu la ufuatiliaji na tathmini. Lengo hapa ni kuhakikisha kuwa taarifa za ufuatiliaji na tathmini kutoka katika Wizara na Taasisi za Serikali zinafanyiwa uchambuzi wa kina pamoja na kutoa mrejesho kuhusu utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha na Mipango kufanyia kazi changamoto ya uhaba wa wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini; kazi za tathmini kufanyika kwa ufanisi na uwepo wa mifumo mingi ya ukusanyaji wa taarifa yenye kuathiri ubora wa takwimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya ujuzi unaohitajika, kufanya tathmini ya mifumo ya ufuatiliaji na tathmini iliyopo kwenye taasisi za Serikali, lakini pia kuandaa kanzi-data ya watumishi wenye utaalamu wa masuala ya ufuatiliaji na tathmini, kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwenye ufuatiliaji na tathmini na kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ili kujenga mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ambao utawezesha kufuatilia, kuchambua na kupata taarifa halisi na kwa wakati za utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na uhifadhi wa mazingira; suala la kulinda na kuhifadhi mazingira limeendelea kuwa moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais katika hotuba zake mbalimbali ndani na nje ya nchi amekuwa akisisitiza umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa jamii yetu na kwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu ambazo siyo endelevu na rafiki wa mazingira zikiwemo ukataji wa miti hovyo, uvamizi na uharibifu wa mapori tengefu, ukataji wa miti holela kwa ajili ya uchomaji wa mkaa, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na uchomaji moto misitu yetu zimekuwa zikichangia sana uharibifu wa mazingira nchini. Jitihada zinazofanywa na Serikali kuhifadhi mapori yetu ni katika kulinda tunu zilizopo kwenye maeneo muhimu kama vile Loliondo, Ngorongoro, Selous, Ruaha, Katavi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Pori Tengefu la Loliondo; Pori Tengefu la Loliondo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 4,000 limekuwa likitumiwa na wananchi kuendesha shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ulishaji wa mifugo na makazi. Serikali kwa upande wake imeendelea kulitumia katika shughuli za uhifadhi na utalii. Aidha, matumizi yasiyo rafiki yamekuwa chanzo cha kuharibika kwa mfumo ikolojia wa pori hilo.

Mheshimiwa Spika, Pori Tengefu Loliondo ni muhimu kwa ajili ya kulinda mfumo ikolojia ya Serengeti, ikiwemo maeneo ya mazalia, makazi na mapito ya makundi makubwa ya nyumbu wahamao. Sababu kubwa ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni kuhifadhi mzunguko wa nyumbu ambao kwa kiasi kikubwa uko upande wa Tanzania na umuhimu wake kama urithi wa dunia. Serikali

imekuwa ikifanya mabadiliko pale ambapo imeonekana mzunguko huu uko hatarini na hivyo kuhakikisha kuwa unalindwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu yanayohitaji kuhifadhiwa kwa lengo la kulinda mzunguko wa nyumbu ni maeneo ya mazalia na mapito kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 za Pori Tengefu la Pololeti lililoko ndani ya Pori Tengefu la Loliondo. Maeneo mengine muhimu ni vyanzo vya maji ambavyo huingiza maji kwenye mito mikuu mitatu ya Nyabogati, Pololeti yenyewe na Grumeti.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa maeneo haya ni muhimu ili kuinusuru ikolojia ya Serengeti ikiwemo Bonde la Seronera ambako mito hii humwaga maji yake na ndicho kitovu cha utalii ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti. Kadhalika eneo hilo la Pololeti lililoko ndani ya Pori Tengefu la Loliondo linalopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, limeendelea kuwa eneo muhimu kwa ajili ya mtawanyiko wa wanyamapori hususan nyumbu, pundamilia na pofu.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na makazi zimekuwa chanzo cha uharibifu wa ikolojia niliyoielezea awali ambayo ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa hifadhi zetu hususan Serengeti. Vilevile shughuli hizo zimechangia uharibifu wa uoto wa asili na kusababisha kukosekana kwa malisho na maji, kupungua uwezo wa kiuchumi kwa wafugaji. Aidha, ongezeko la mifugo limesababisha maeneo yote ya vyanzo vya maji na mito kuharibika. Uharibifu huo mkubwa wa mazingira, pia umekuwa chanzo cha wanyamapori kutoweka.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uwepo wa matumizi endelevu ya Pori Tengefu la Loliondo, Serikali ilielekeza eneo la kilometa za mraba 1,500 lihifadhiwe na eneo lililobaki la kilometa za mrada 2,500 wananchi waendelee kulitumia kwa shughuli zote za kijamii. Utekelezaji

wa maelekezo hayo ya Serikali umehusisha zoezi la kuwekwa vigingi katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,500 la Pori Tengefu Pololeti lililoko kwenye Pori Tengefu la Loliondo.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la uwekaji wa vigingi ambalo limekamilika kwa asilimia 100 haliathiri maendeleo ya wakazi wa eneo la vijiji 14 vinavyopakana na eneo hilo. Aidha, hakutakuwepo na kijiji kitakachofutwa na hakuna miundombinu itakayoondolewa kwa kuwa ndani ya eneo la kilometa za mraba 1,500 la Pololeti hakuna miundombinu yoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesimamia kwa umakini mkubwa zoezi hili la uwekaji vigingi kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 ambalo ni muhimu kwa ikolojia ya Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Halikadhalika Serikali imeendelea kushirikiana na wananchi wa Loliondo katika kuboresha malisho ya mifugo, uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa majosho pamoja na miundombinu ya kunyweshea mifugo kwenye eneo la kilometa za mraba 2,500.

Mheshimiwa Spika, pia naielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na wadau wengine kuhakikisha kuwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 inatumika ipasavyo kutenga na kuweka mipaka ya vijiji. Serikali kwa kuzingatia matakwa ya wananchi hasa maeneo ya malisho kwenye vijiji 14 vilivyopo karibu na Pori Tengefu la Poloreti itaweka utaratibu utakaopangwa kwa pamoja baada ya kukamilisha zoezi la utambuzi wa mifugo kwenye vijiji husika kwa lengo la kuwezesha kuhudumia mifugo iliyopo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Ngorongoro; tangu kuanzishwa kwa matumizi mseto ya ardhi takribani miaka 60

iliyopita, usimamizi wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro umeshindwa kutimiza lengo la kuleta uwiano baina ya uhifadhi, ukuzaji wa utalii na maendeleo ya jamii kutokana na changamaoto mbalimbali. Hali hiyo imechangiwa na changamoto nyingi za kiuhifadhi na maendeleo ya jamii hususan ongezeko la idadi kubwa ya watu na mifugo, makazi holela na shughuli za binadamu. Kwa mfano, mwaka 1959 wakati hifadhi hiyo inaanzishwa kulikuwa na watu takribani 8,000 na mifugo 161,000. Lakini leo hii idadi ya watu inakadiriwa kuwa takribani 110,000 na mifugo zaidi ya 1,000,000. Ni jukumu la Serikali kuweka miongozo itakayowezesha maisha ya watu na uhifadhi kuwa endelevu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kuendelea kudorora kwa ustawi wa maisha ya wenyeji wa Ngorongoro katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo elimu, afya, uchumi, usalama wa chakula na lishe, ufinyu wa vyanzo mbadala vya mapato kwa jamii, makazi duni, kukosa haki ya msingi ya kikatiba ya kumiliki na kutumia ardhi kwa ajili ya maendeleo yao kwa sheria zilizopo. Pia kumejitokeza kubadilika kwa uoto wa asili na kuenea kwa mimea vamizi. Hivyo kuendelea kuwepo kwa mfumo uliopo, utaathiri ustawi endelevu wa maliasili ambazo ndio chanzo kikubwa cha mapato ambayo hugharamia shughuli za maendeleo na ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Serikali kwa nyakati tofauti ilichukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto za usimamizi wa hifadhi ikiwemo kufanya tathmini ya kina tangu mwaka 2017 hadi mwaka 2021 kwa lengo la kutatua changamoto za mfumo wa matumizi mseto ya ardhi. Kutokana na tathmini hiyo, Serikali iliamua kutumia Mapori Tengefu ya Handeni na Kitwai yaliyopo katika Wilaya za Handeni na Kilindi kwa ajili ya wananchi wa Ngorongoro kuhamia na kuendeleza maisha yao na kujitafutia shughuli mbalimbali za uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya kutumia maeneo ya Handeni na Kitwai ni pamoja na kufaa kwa ufugaji na kilimo, mwingiliano wa kimila, kitamaduni na desturi katika ya jamii iliyopo Handeni na Kitwai na jamii ya wafugaji wa Ngorogoro na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo zinafanana sana ambapo shughuli kuu ni ufugaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanakidhi makusudio yaliyotarajiwa, Serikali imeendelea kujenga miundombinu muhimu katika eneo la Msomera ikiwemo upangaji na upimaji wa viwanja vya makazi na mashamba na ujenzi wa nyumba 500 za wakazi ambapo ujenzi wa nyumba 103 umekamilika na ujenzi wa nyumba 400 unaendelea kupitia JKT. Vilevile huduma za umeme na maji tayari zinapatikana na ujenzi wa shule ya msingi na sekondari umekamilika. Ujenzi wa miundombinu ya afya, majosho na barabara unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa za eneo la Msomera lililopo Handeni kiuchumi na kijamii kupitia vikao vingi na wananchi wa eneo la Ngorongoro wakiwemo viongozi wa mila Laigwanak na Laigwarad, Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wa Kata na Vijiji, wawakilishi wa akinamama, vijana, wazee na wadau wengine. Hadi sasa kumekuwa na mafanikio makubwa katika kusimamia utekelezaji wa zoezi hilo ambapo Serikali imeendelea kuhamasisha na kuandikisha zile kaya ambazo zipo tayari kuhama kwa hiari yao.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuandikisha wakazi wanaoomba kuhama kwa hiari linaendelea vizuri. Aidha, hadi kufikia tarehe 9 Juni, jumla ya kaya 293 zenye watu 1,497 zilikuwa zimeshajiandikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wakazi wanaohama wanakuwa na maisha bora zaidi katika makazi

mapya Msomera, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia kutoa motisha mbalimbali kwa wakazi hao kama ifuatavyo:-

(i) Kila kaya inayoondoka inapewa fidia ya nyumba aliyokuwa anaishi;

(ii) Kaya zote zinazohamia Msomera kwa hiari zinapatiwa nyumba zenye vyumba vitatu zilizojengwa kwenye eneo la ekari 2.5, wanapewa godoro, wanapewa tochi, wanapewa na ndoo;

(iii) Kila kaya inapewa shamba lenye ukubwa wa ekari tano kwa ajili ya malisho na zitakabidhiwa hati za kumiliki ardhi hiyo kwa ajili ya eneo la nyumba na shamba. Mbali ya eneo hilo la kulishia kuna eneo la wazi la kuchungia nalo ni huru kwa kuchungia;

(iv) Kila kaya inapewa fedha ya kutosha kwa ajili ya kuanzia maisha kwenye makazi mapya ya Msomera; na

(v) Kila kaya inapewa mahindi magunia mawili kwa kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya kujikimu katika kipindi cha mpito wakati wakazi wakijiandaa na maandalizi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upendo huo uliooneshwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu hauna budi kupongezwa na kila mwenye kuitakia mema nchi hii. *(Makofi)*

Hata hivyo, utaratibu huu ni maalumu kwa Ngorongoro pekee. Leo tarehe 30 Juni, 2022 kaya nyingine 25 zenye jumla ya watu 115 zinatarajiwa kuanza safari asubuhi hii kwa hiari yao kuelekea Msomera na kuendelea na maisha yao kama kawaida. Nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wote walioridhia kuhama kwa hiari yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Juni, 2022 nilitembelea Ngorongoro na nilipata fursa ya kuwaaga wananchi wanaohama kwa hiari yao kutoka katika Hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera. Aidha, siku hiyo hiyo, nilitembelea eneo la Msomera lililopo Wilaya ya Handeni na kujionea wananchi waliohamia katika eneo hilo wakiendelea na shughuli zao kwa furaha na amani ambapo waliishukuru sana Serikali na walimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuwaandalia makazi bora katika eneo hilo. Kwa ridhaa yako ninaomba tuwasikilize hao wachache. *(Makofi)*

*(Hapa video ya wananchi waliohamia Msomera ilioneshwa Bungeni)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, niendelee nitoe rai kwa viongozi na watendaji kuendelea kuelimisha, kuhamasisha na kuwashirikisha wananchi na wadau wengine hususan wenyeji katika utekelezaji mzuri unaoendelea wa zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upandishwaji hadhi wa maeneo ya mapori tengefu kuwa mapori ya akiba; rasilimali za wanyamapori ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, hususan katika kukuza utalii na hivyo kuongeza pato la Taifa. Kwa msingi huo, mpango wa Serikali kupandisha hadhi baadhi ya mapori tengefu kuwa mapori ya akiba ni katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali zilizopo katika mapori hayo kwa uhifadhi endelevu. Hata hivyo, kutangazwa kwa eneo lolote lile kuwa pori la akiba hufanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufuata taratibu zilizowekwa kisheria ikiwemo kufanya tathmini ya kina ya umuhimu wa eneo hilo katika kuhifadhi na kushirikisha wananchi waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, tathmini hiyo na ushirikishwaji wa wananchi husaidia Serikali kufanya maamuzi ya iwapo

kuendelea na utaratibu wa kupandisha hadhi au la. Hivyo naomba niwahakikishie wananchi wa maeneo husika ikiwemo eneo la Loliondo kwamba utaratibu wa kupandisha hadhi maeneo ya mapori hayo kuwa mapori ya akiba utasubiri mapitio ya pamoja kati ya Serikali na wananchi. Hivyo Wizara isianze kazi hiyo ili kupata maoni ya wadau na wananchi watoe maoni yao kwa maslahi ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo; katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali imeongeza bajeti yake ya Wizara ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294 katika mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 954 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 224 na limelenga kwenye maeneo yafuatayo; moja, utafiti wa kilimo; lakini pia uzalishaji wa mbegu; tatu, umwagiliaji; nne, ujenzi wa maghala; na tano kuimarisha huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali hapa ni kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 (Ajenda 10/30), kuongeza mauzo nje ya nchi kutoka dola za Marekani bilioni 1.2 hadi kufikia dola za Marekani bilioni tano kwa mwaka 2030, kupunguza umaskini kwa zaidi ya asilimia 50 kutoka asilimia 28 kwa sasa hadi chini ya asilimia 14 ifikapo 2025.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo, Serikali imepanga kuimarisha utafiti, kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano na miche ya chikichi, kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo utakaowezesha upatikanaji wa pembejeo kwa mfuko wa ruzuku pindi inapotokea athari za kiuchumi na kuanza kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bajeti kwa mwaka 2022/2023 linatarajiwa kuimarisha usalama wa chakula na lishe na hivyo kupunguza mfumuko wa bei ya chakula nchini, kuongeza eneo la umwagiliaji; kuongeza upatikanaji wa ajira kwa vijana na wanawake katika kilimo zitakazofikia milioni moja ifikapo mwaka 2025. Manufaa mengine ni kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo kufikia asilimia 100 ifikapo 2030.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na athari za kupanda kwa bei ya mbolea duniani, Wizara itaimarisha mfumo wa utoaji ruzuku ambapo tunatarajia kutumia shilingi bilioni 150 kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote. Kwa kipekee kabisa mfumo wa utoaji wa ruzuku utawalenga wazalishaji wa ndani. Aidha, kipekee makampuni ambayo hayataungana na Serikali katika mfumo huu Serikali hatutosita kuwafutia leseni ya kuendesha biashara ya mbolea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, maelekezo mahsusi; ni dhahiri kuwa hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, zimekuwa na zinakusudia kuleta matokeo chanya na ya haraka kwenye nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa msingi huo, nami ningependa kusisitiza na kuelekeza utekelezaji wa masuala yafuatayo: -

(i) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na mamlaka mbalimbali za Serikali inazungumza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio mbalimbali katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA ikiwemo kuunganisha taasisi zaidi ya 700 katika mfumo mmoja wa malipo *GePG*. Hivi sasa Serikali inaweza kuona na kupata taarifa za makusanyo yote yaliyokusanywa kwenye taasisi

zake kupitia mfumo uliounganishwa na mifumo mingine kama vile *MUSE, GAMIS, TANePS, ERMS, HCMIS, LGRCIS,* mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* pamoja na mifumo ya Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio hayo makubwa Serikali imejenga mfumo maalum unaojulikana kama *Government Enterprise Service Bus (GovESB)* kwa ajili ya kuwezesha mifumo mbalimbali ya Mamlaka na Taasisi za Serikali kubadilishana taarifa na kuzungumza. Kwa msingi huo, niwaelekeze Wizara ya Fedha ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na wadau wengine muhimu kutekeleza haya ambayo ninaelekeza.

(i) Kuhimiza taasisi za umma kuunganisha mifumo yao ya TEHAMA kupitia mfumo huu maalum;

(ii) Kusimamia ujenzi wa mfumo wa *Universal Billing System* utakaotumiwa na taasisi ambazo hazina uwezo wa kujenga mifumo yao; na

(iii) Kuhakikisha taasisi za umma zinajielekeza zaidi katika matumizi ya mifumo shirikishi pale ambapo taratibu za kiutendaji kazi zinafanana badala ya kila taasisi kujenga mfumo wake. Lakini kubwa la pili ni viongozi na watendaji wa Serikali kuisemea na kutangaza mafanikio ya Serikali kwenye maeneo yao na sekta husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanazuoni wamewahi kusema kuwa uongo ukisemwa mara nyingi hugeuka kuwa ukweli. Nimeamua kurejea kauli hiyo kutokana na ukweli kwamba uzoefu wa mwaka mmoja wa uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaonesha kuwa yapo mafanikio lukuki tuliyoyapata kama nchi katika kipindi hicho. Hata hivyo licha ya ukweli huo bado wananchi hawajaelezwa ipasavyo na wakati mwingine tumeacha upotoshaji ukiendelea

kufanywa bila kusahihishwa au kuchelewa sana kusahihisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa ni jukumu letu viongozi na watendaji wote kuhakikisha kwamba wananchi wanaelezwa kuhusu shughuli zinazofanywa na Serikali, mafanikio na changamoto zilizopo na pia mwelekeo wa viongozi wetu na watendaji wote kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kupata taarifa za Serikali kuhusu juhudi mbalimbali za kuwaletea maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kutoa bure, elimu msingi bila ada; nitumie nafasi hii tena kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake na dhamira njema ya kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2020 kuhusu Serikali kutoa elimu msingi bila ada kwa ngazi ya elimu ya shule za msingi hadi sekondari kidato cha sita yenye kulenga kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu, mahudhurio na ufaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mpango huu, Waheshimiwa Wabunge wamelalamikia sana kuwepo kwa utitiri wa michango shuleni. Aidha, Serikali kupitia Waraka wa Elimu Namba 5 wa mwaka 2015 na Waraka wa Elimu Namba 6 wa mwaka 2015 imetoa maelekezo bayana kuhusu utekelezaji wa elimu msingi bila malipo ikiwemo matumizi ya fedha za utawala ambazo hutolewa Hazina na kupelekwa moja kwa moja katika akaunti za shule za husika za msingi na sekondari kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati, uendeshaji wa mitihani ya ndani na utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 10 ya fedha hiyo pia hutumika kugharamia huduma za umeme, maji na ulinzi.

Hivyo basi ninaagiza kuwa TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kufuatilia matumizi na upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha hizo pamoja na kuhakikisha kwamba hakuna michango holela inayotozwa kwa wanafunzi. Aidha, kuanzia sasa hakikisheni maelezo ya kujiunga na shule za umma yaani *joining instructions* yanahakikiwa na kupewa idhini na Katibu Tawala wa Mkoa husika kwa kushirikiana na Maafisa Elimu wa Wilaya ikiwa inatamka kuwa hakuna michango yoyote ya holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; eneo la mwisho ambalo ningependa kulitolea msisitizo ni utekelezaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Kama mnavyofahamu tarehe 23 Agosti, 2022 imepangwa kuwa siku ya Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022. Zoezi hilo lilitanguliwa na Operesheni ya Anwani za Mfumo wa Makazi ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 95 na Serikali imefanikiwa kukusanya taarifa na kutoa anwani za makazi zaidi ya milioni 12.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi ninaelekeza kama ifuatavyo:-

(i) Taasisi zote zenye dhamana ya masuala ya ardhi na makazi kuhakikisha zinakuja na mikakati thabiti ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyoainishwa wakati wa utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi pamoja na kutoa miongozo ya namna bora ya kushughulikia changamoto za Watanzania wenzetu kuishi katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria ili kuhakikisha kwamba wananchi hao wote wananufaika na fursa hizi za kuwa na anuani ya makazi; *(Makofi)*

(ii) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhakikisha kuwa Mpango wa Uendelezaji wa Mfumo

*(System Sustainability Framework)* unaotoa mwongozo wa shughuli zote za anwani za makazi zitakavyofanyika unatumika vizuri ili kufanya zoezi hili kuwa na thamani wakati wote;

(iii) Viongozi katika ngazi zote husussan kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wahakikishe kuwa jamii inaendelea kuelimishwa ili kujua manufaa sanjari na kulinda miundombinu ya anwani za makazi kwenye maeneo yao;

(iv) Wizara zote, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa endeleeni kushughulikia changamoto zote zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi na kuhakikisha kwamba zoezi hilo linakuwa endelevu; na

(v) Uhakiki wa majina ya mitaa katika vibao uendelee kufanyika ili kujiridhisha usahihi wake na muonekano kwa mbali lakini pia kuhakikisha kwamba inaonesha kwamba ni barabara ipi, nyumba ipi namba ngapi na kama ambavyo imeelekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 yanaendelea vizuri na yamefikia asilimia 87. Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu hususani mnaporejea kwenye maeneo yenu ya uwakilishi kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye zoezi hilo muhimu la sensa. Lakini vilevile nitoe wito kwa Watanzania wote kujiandaa kuhesabiwa ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Makarani wa Sensa na viongozi wetu kwenye maeneo tunayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* kwa

kupaisha mchezo wa soka nchini na kuifanya ligi ya Tanzania kuwa kivutio kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka nitumie nafasi hii kuipongeza Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 maarufu kama *Serengeti Girls* kwa kufuzu kushiriki michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika Oktoba, 2022 nchini India. Tunawatakia kila la heri wawakilishi wetu hao ambao wataungana na Morocco na Nigeria kuiwakilisha Afrika na kukamilisha idadi ya timu 16 zinazoshiriki fainali hizo za dunia zikiwa ni fainali za saba tangu michuano hiyo ilipoasisiwa mwaka 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Timu ya Taifa ya Walemavu ya Mpira wa Miguu *(Tembo Warriors)* kwa kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwezi Oktoba, 2022 nchini Uturuki. Nitoe wito kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana kwa karibu na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kuwezesha maandalizi mazuri kwa timu zote mbili kuelekea mashindano hayo ya dunia ili tukashindane na kuitangaza vema Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa upande wa michezo niwapongeze basi *Dar Young Africans* - Wananchi kwa kuibuka vinara wa Ligi Kuu ya *NBC* msimu wa 2021, hongereni sana, mmekuwa na msimu mzuri na mmestahili kuibuka kuwa mabingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spik,a miongoni mwa matukio yaliyonivutia wakati wa shamrashamra za Ubingwa wa wananchi ni kitendo chao cha kukumbuka kuitangaza Tanzania kupitia *Royal Tour* na kuhamasisha ushiriki wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Kama ambavyo klabu ya soka ya Simba ilivyoanzisha kuitangaza Tanzania kwenye medani za soka za kimataifa kupitia jezi zao kwa kuandikwa *Visit Tanzania*. Niendelee kutoa wito kwa vilabu na makundi ya

Watanzania wanaosafiri nje ya nchi kuhakikisha kwamba wanatumia jezi zetu zenye kubeba jumbe au ajenda za kitaifa kwani jukumu la kuitangaza Tanzania na ajenda zake za kitaifa ni jukumu letu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, niwatakie safari njema Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnaporejea majimboni mwenu. Niwaombe mtakapokuwa huko majimboni muwaeleze wananchi mambo yaliyojiri hapa Bungeni wakati wote wa Mkutano wa huu wa Saba wa Bunge hili la Kumi na Mbili, matarajio yetu kwao na kuwasihi kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita kwenye jitihada zake za kuwawekea mazingira wezeshi ya kujikwamua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia, watendaji wa Serikali ambao uweledi na ufanisi mkubwa waliouonesha umekuwa chachu katika kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu. Vilevile niwashukuru wanahabari kwa kufikisha habari za Mkutano huu kwa wananchi. *(Makofi)*

Kipekee, nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama, huduma wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili bila kuwasahau madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Lakini pia nisimsahau Katibu wa Bunge pamoja na watumishi wa Bunge kwa kutuhuduma vizuri wakati wote tukiwa hapa Bungeni, hakika huduma tuliyoipata imetufurahisha sote na imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu tukiwa hapa Bungeni  kwa kipindi chote cha miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba tarehe 10 Julai, 2022 kutegemea mwandamo wa mwezi, kutakuwa na sikukuu ya *Eid El Hajj.* Nitumie fursa hii kuwatakia ndugu zetu

waislamu na Watanzania wote nchini maadhimisho mema ya sikukuu hiyo ya *Eid El Hajj. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu liahirishwe hadi tarehe 13 Septemba, 2022 siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI AKITOA HOJA YA KUAHIRISHA MKUTANO WA SABA WA BUNGE LA 12 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 30 JUNI, 2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**Shukurani**

1. ***Mheshimiwa Spika*, awali ya yote**, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuhitimisha shughuli zote za Mkutano wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa buheri wa afya.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vema mijadala ya Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili. Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami kwamba katika kipindi hiki kifupi tangu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini ashike wadhifa wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha ukomavu, uhodari na umakini mkubwa katika kuliongoza Bunge hili tukufu.

3. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ninawapongeza sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalumu kwa kuonesha umahiri na weledi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kuhakikisha shughuli zote za mkutano huu zinakamilika kama zilivyopangwa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa hoja za bajeti za Wizara zao, kutoa ufafanuzi wa kina pamoja na kujibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mijadala ya hoja hizo. Ni matumaini yangu kwamba baada ya kuhitimishwa kwa shughuli za Mkutano huu, sasa watakwenda kusimamia ipasavyo sekta zao ili kuhakikisha bajeti zilizowasilishwa zinagusa maeneo ya msingi na maslahi mapana ya Watanzania.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitotambua ushiriki mzuri na michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzagu wakati wote wa Mkutano huu tangu ulipoanza tarehe 5 Aprili 2022. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwani michango na ushiriki wenu umekuwa chachu katika kufanikisha shughuli za Mkutano wa Saba wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan katika kutekeleza kikamilifu wajibu wetu wa Kikatiba wa kupitia, kujadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii, kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kwa upande wake itazingatia maoni na ushauri wao kwa ajili ya kulinda maslahi mapana ya Watanzania. Aidha, nitoe wito kwa

Waheshimiwa Wabunge kuwa katika kipindi hiki tunaporejea majimboni kwetu tukawe mabalozi wazuri kwa wananchi tunaowatumikia kuhusu mambo mengi muhimu yaliyojiri katika kipindi chote cha Mkutano huu hususan mipango na mwelekeo wa Serikali katika kipindi cha mwaka 2022/2023.

**Salamu za Pole**

7. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 24 Aprili 2022 wakati tukiendelea na shughuli za Mkutano wa Saba wa Bunge lako tukufu, tulipokea taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Irene Ndyamukama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia Chama cha Mapinduzi kilichotokea katika Hospitali ya Tumbi iliyopo Kibaha, mkoani Pwani. Hivyo basi, nami kwa masikitiko makubwa naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwako Mheshimiwa Spika, kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kufuatia kuondokewa na mpendwa wetu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, pia tumeshuhudia kutokea kwa ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri zikihusisha pikipiki, magari, treni n.k. Ajali hizo, zimesababisha vifo vya wapendwa wetu, uharibifu wa mali na pengine ulemavu. Kwa msingi huo, nitoe pole kwa Watanzania wenzangu waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata majeraha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo matukio ya ajali za vyombo vya usafiri. Niwatakie afya njema na uponyaji wa haraka wale wote waliojeruhiwa na tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

**SHUGHULI ZA BUNGE**

9. ***Mheshimiwa Spika*****,** sambamba na kupitia, kujadili na hatimaye kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023, Bunge lako tukufu pia lilipata fursa ya kupokea maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kutolewa

majibu kutoka upande wa Serikali. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni kujadili na kupitisha miswada ya sheria, maazimio ya Bunge na kupokea kauli za Serikali katika kutolea ufafanuzi hoja kadhaa zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge ambazo zilihitaji kupata kauli ya Serikali.

**Maswali na Majibu**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano wa Saba wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jumla ya maswali **487** ya msingi na mengine **2,622** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Halikadhalika, jumla ya maswali **27** ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Miswada**

11. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya Miswada ya Sheria **minne** iliweza kujadiliwa na kupitishwa na Bunge lako tukufu. **Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2022** na **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022** ilisomwa kwa mara ya kwanza.

12. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, **Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022** na **Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali** ilisomwa kwa hatua zake zote.

**Maazimio**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bunge lako tukufu lilifanikiwa kujadili na kupitisha Maazimio matatu ya Bunge yafuatayo:-

i. Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kuwa miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani na kupewa tuzo ya juu ya Mjenzi Mahiri ya Babacar Ndiaye kufuatia mafanikio makubwa katika ujenzi wa miundombinu;

ii. Azimio la Bunge la kuipongeza timu ya Taifa ya wanawake ya mpira wa miguu (Serengeti Girls) baada ya kufuzu michuano ya kombe la dunia itakayofanyika nchini India; na

iii. Azimio la Bunge la kuipongeza timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wenye Ulemavu (Tembo Warriors) kufuatia kufuzu michuano ya kombe la dunia itakayofanyika nchini Uturuki.

**Kauli za Serikali**

14. ***Mheshimiwa Spika**,* kwa kuzingatia Kanuni ya 56 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2020, Waheshimiwa Mawaziri walitoa kauli rasmi za Serikali Bungeni ikiwa ni ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja hizo, zilihusu baadhi ya mambo yaliyotokea nchini na kugusa moja kwa moja maslahi ya wananchi. Kauli zilizotolewa ni kama ifuatavyo: -

(i) **Wizara ya Nishati**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mkutano huu Mheshimiwa Januari Yusuf Makamba (Mb.), Waziri wa Nishati alitoa Kauli ya Serikali Bungeni kuhusu kupanda kwa bei za mafuta na hatua zinazochukuliwa kushughulikia suala hilo. Serikali pamoja na mambo mengine ilitoa mwenendo wa bei ya mafuta, mipango ya muda mfupi na mrefu ya kukabiliana na changamoto hiyo pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa ikiwemo kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 ili kupunguza makali ya bei ya mafuta nchini.

(ii) **Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mheshimiwa Hamad Masauni (Mb.), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa Kauli ya Serikali Bungeni kuhusu **Watanzania waliopo Nje ya Nchi kurudi nchini kushiriki shughuli za Ujenzi wa Taifa**. Kauli hiyo, imezingatia hali nzuri ya kisiasa na kiusalama nchini pamoja na hatua za dhati zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kila mtanzania wakiwemo viongozi wa kisiasa waliopo ndani na nje ya nchi wanashiriki katika shughuli za ujenzi wa nchi yao.

**MWELEKEO WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** leo tunaelekea kuhitimisha shughuli za Mkutano wa 7 wa Bunge la Kumi na Mbili. Aidha, kupitia Mkutano huu, pamoja na mambo mengine Bunge lako tukufu limefanikiwa kupitia, kujadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Bajeti tulioipitisha imeendelea kututhibitishia nia njema, uthubutu wa hali ya juu na azma ya kweli ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutelekeza mipango na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwaletea watanzania maendeleo ya haraka sambamba na kuwakwamua kiuchumi.

18. ***Mheshimiwa Spika***, mengi yameelezwa na kufafanuliwa na Waheshimiwa Mawaziri wakati wakiwasilisha hoja za bajeti za sekta zao, na wakati mwingine hata Waheshimiwa Wabunge wakati walipokuwa wakichangia hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kupitia kwa Waheshimiwa Mawaziri. Kwa lugha nyingine, kupitia hotuba hii ya kuhitimisha shughuli za Serikali zilizopangwa kwenye Mkutano wa 7 wa Bunge la 12, nisingependa kurudia kile kilichokwisha jadiliwa wakati wote wa Mkutano huu.

19. ***Mheshimiwa Spika***, hata hivyo, niruhusu nitumie fursa hii kugusia kwa uchache baadhi ya mambo ya msingi ambayo yanaakisi taswira, dhamira, nia, uthubutu, maono na azma ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha taifa letu linapiga hatua za haraka za maendeleo ndani ya kipindi kifupi. Miongoni mwa mambo hayo ni ujio wa Filamu ya Royal Tour; ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 na kuwekwa saini kwa Makubaliano ya Awali ya Utekelezaji wa Mradi wa Usindikaji Gesi Asilia (LNG).

**Filamu ya Royal Tour**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako tukufu litakubaliana nami kwamba sekta ya utalii imeendelea kupata mafanikio makubwa hususan kufuatia uzinduzi wa filamu ya Royal Tour tarehe 28 Aprili, 2022 Jijini Arusha. Filamu hiyo ya kihistoria imekuja katika kipindi muhimu ambacho sekta ya utalii na huduma ilikumbwa na athari za UVIKO-19. Hivyo, ujio wa filamu hiyo, umechangia kuimarisha shughuli za utalii na kusaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa sintofahamu nyingi kuhusu urithi wa utalii uliopo Tanzania. Mheshimiwa Rais ameweza kuonesha uhalisia wa nchi yetu kuanzia vivutio vya biashara, utalii, madini na hata sanaa na utamaduni wetu.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** matunda ya jitihada hizo za Mheshimiwa Rais yameanza kuonekana hususan kwenye sekta ya utalii na huduma ambapo watalii na wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali duniani wameanza kumiminika nchini. Mathalan, watu maarufu wakiwemo wachezaji wa mpira wa miguu kutoka ligi kuu mashuhuri barani ulaya na ligi ya mpira wa kikapu nchini Marekani wametembelea Tanzania katika kipindi hicho. Kadhalika, wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii yakiwemo Marekani, Israeli, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kuja nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao.

22. ***Mheshimiwa Spika****,* katika hatua nyingine, mwezi Aprili, 2022 Serikali iliingia makubaliano na Jiji la Dallas lililopo nchini Marekani kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya utalii, biashara na uwekezaji. Hatua hiyo, inalenga kufungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani.

23. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali ya utalii nchini ili kufikia lengo la kuvutia watalii milioni 5 kwa mwaka sambamba na mapato ya Dola za Marekani bilioni 6 ifikapo mwaka 2025. Kuongezeka kwa idadi ya wageni wanaotembelea Tanzania, kutaimarisha sekta ya utalii na huduma nchini na hivyo, kutengeneza fursa nyingi zaidi za ajira, kuwakwamua wananchi kiuchumi na kujenga uchumi imara na shindani.

**Ujenzi wa Miradi ya Maji katika Miji 28**

24. ***Mheshimiwa Spika*, **itakumbukwa kuwa tangu akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa alijipambanua na mpango maarufu wa **kumtua ndoo mama kichwani**. Dhamira hiyo ya Mheshimiwa Rais imeendelea kujidhihirisha kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28 uliozinduliwa tarehe 6 Juni, 2022.

25. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi huo wenye thamani ya Dola za Marekani **milioni 500** utachangia kwa kiwango kikubwa katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye miji iliyobainishwa ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mradi huo wa maji ambao ni mkubwa zaidi kuwahi kutekelezwa nchini kwa wakati mmoja, utakapokamilika utahakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa wananchi wapatao **milioni sita.**

26. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, miradi hiyo pia itakuwa chachu kwenye kuvutia uwekezaji hususan wa viwanda. Serikali kwa upande wake, itahakikisha kuwa ujenzi wa miradi ya maji kwenye miji 28 unafungua fursa nyingine za kiuchumi zikiwemo ajira kwa wananchi wetu hasa kwenye maeneo ambayo miradi hiyo itatekelezwa. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuwasihi watanzania wenzangu kuchangamkia fursa zitakazojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi.

27. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mantiki hiyo, niwasihi viongozi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushirikiane katika kuimarisha usimamizi wa miradi hii pamoja na kuhakikisha wakandarasi wanakamilisha miradi hiyo kwa wakati ili miradi hiyo iweze kutoa huduma iliyotarajiwa kwa wananchi. Vilevile, niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa vinara katika kuhamasisha wananchi kutunza mazingira na kuacha kufanya shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji kwani uhifadhi wa mazingira ndiyo msingi wa uendelevu wa upatikanaji wa majisafi na salama.

**Utekelezaji wa Mradi wa Usindikaji Gesi Asilia (LNG)**

28. ***Mheshimiwa Spika*,** sote tumekuwa miongoni mwa mashuhuda wa kusuasua kwa muda mrefu kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa uchakataji wa Gesi Asilia (LNG). Kwa msingi huo, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikiwa kutegua kile kitendawili cha muda mrefu cha lini ungeanza utekelezaji wa mradi wa uchakataji wa Gesi Asilia (LNG) uliosimama kwa muda mrefu.

29. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, tarehe 11 Juni, 2022 tulishuhudia kuingiwa kwa makubaliano ya awali ya Mkataba wa Nchi

Hodhi na Kampuni za Kimataifa za Utafutaji Mafuta kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa LNG.

30. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais inatimia nitumie fursa hii kutoa wito kwa viongozi na watendaji wa sekta husika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi wa LNG unaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa taifa letu ikiwa ni pamoja na kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na mauzo ya gesi, kuzalisha ajira za muda mfupi na za kudumu na kuimarisha mapato na uchumi wa watanzania kupitia mauzo ya bidhaa na huduma mbalimbali wakati wa utekelezaji wa mradi.

31. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa upande wake itaendelea kuhakikisha kuwa inavutia uwekezaji unaokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya Dola za Marekani bilioni 30 kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Vilevile, ninaielekeza Wizara ya Nishati kuhakikisha kuwa inatumia vema fursa ya uwepo wa mradi wa LNG kuimarisha uzoefu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini (TPDC) katika shughuli za gesi pamoja na kuwezesha upatikanaji wa gesi asilia iliyochakatwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

## UJENZI WA MJI WA SERIKALI

32. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, Mheshimiwa Rais aliridhia takriban shilingi **bilioni 600** zitumike kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo 25 ya wizara na taasisi kwenye Mji wa Serikali uliopo Mtumba jijini Dodoma. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba ujenzi huo unaendelea vizuri na hadi kufikia tarehe 24 Juni 2022 umefikia kati ya wastani wa asilimia 30 hadi asilimia 56.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kuzihimiza wizara na taasisi kuhakikisha wanaimarisha usimamizi ili ujenzi ukamilike ndani ya muda uliopangwa. Nitoe rai pia kwenu

Waheshimiwa Wabunge mnapoondoka hapa Bungeni mpate muda kidogo wa kutembelea na kuona kazi nzuri inayoendelea kwenye mji huo.

**UWAJIBIKAJI KATIKA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha dhamira nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa inayojiakisi kwenye Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 inafikiwa, Serikali imejipanga vema kuendelea kusimamia suala la uwajibikaji katika utumishi wa umma. **Mikakati iliyopo katika kuimarisha uwajibikaji hususan kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo: -**

**Moja:** Kuongeza bajeti ya matumizi mengineyo katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutoka **shilingi bilioni 57.44** hadi **shilingi bilioni 79.09** ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hizo. Sambamba na ongezeko hilo la Bajeti katika mwaka 2022/2023, Serikali pia, imehuisha muundo wa Sekretarieti za Mikoa kwa kuboresha iliyokuwa Sehemu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa na kuwa Sehemu ya Menejimenti, Ufuatiliaji na Ukaguzi ili kuimarisha ufuatiliaji wa mapato, matumizi na utekelezaji wa miradi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

**Mbili**: Kuendelea kuwajengea uwezo Waheshimiwa Mameya, Wenyeviti wa Halmashauri na Miji, Madiwani, Mafisa Tarafa na Watendaji wa Kata kupitia Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo ni kuongeza uelewa wa majukumu yao kisheria, kuimarisha mahusiano yao na viongozi wa kisiasa na kusimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao pamoja na ukusanyaji wa mapato; na

**Tatu**: Kupima utendaji wa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kwa kutumia viashiria muhimu hususan usimamizi wa

mapato na makusanyo ya ndani, upelekaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo, usimamizi wa mikopo ya asilimia 10 ikiwa ni pamoja na marejesho, usimamizi wa miradi ya maendeleo na uzuiaji na utekelezaji wa hoja za ukaguzi zinazoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

**MASUALA YA UFUATILIAJI NA TATHMINI**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo jingine lenye lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji Serikalini ni tasnia ya ufuatiliaji na tathmini. Tasnia hii mtambuka inahitaji uwepo wa mifumo na miundo imara ambayo itawezesha kujenga msingi thabiti wa usimamizi wa utendaji kazi wa Serikali. Kwa kuzingatia hilo, Serikali inaendelea kujenga mifumo na miundo wezeshi katika eneo la ufuatiliaji na tathmini ili kuboresha utendaji kazi unaojali matokeo.

36. ***Mheshimiwa Spika***, hatua hizo zinajumuisha kupitia upya miundo na majukumu ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika eneo la ufuatiliaji na tathmini ili kuziimarisha pamoja na kujenga uwezo wa watumishi katika eneo hilo.

37. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine Serikali imeanza maandalizi ya Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa kuzihusisha taasisi simamizi zinazohusika na ufuatiliaji na tathmini ili kuchambua maeneo wanayosimamia na kuhakikisha maeneo yote muhimu yanajumuishwa ikiwemo usimamizi wa mipango ya maendeleo na utendaji wa Serikali kwa ujumla.

38. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hatua hizo, tayari, Serikali imekamilisha Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ambao utaanza kutumika Julai, 2022.

Mfumo huo, pamoja na mambo mengine utasaidia Serikali kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuongeza tija na thamani ya matumizi ya fedha za umma kwenye miradi husika.

39. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imehuisha Muundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Ofisi ya Waziri Mkuu hususan kwa upande wa Sera, Uratibu na Bunge ili kuimarisha jukumu la ufuatiliaji na tathmini. Lengo ni kuhakikisha taarifa za ufuatiliaji na tathmini kutoka katika wizara na taasisi za Serikali zinafanyiwa uchambuzi wa kina pamoja na kutoa mrejesho kuhusu utendaji wa Serikali.

40. ***Mheshimiwa Spika***, nitoe wito kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha na Mipango kufanyia kazi changamoto ya uhaba wa wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini; kazi za tathmini kufanyika kwa ufanisi na uwepo wa mifumo mingi ya ukusanyaji wa taarifa yenye kuathiri ubora wa takwimu.

41. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya ujuzi unaohitajika, kufanya tathmini ya mifumo ya ufuatiliaji na tathmini iliyopo kwenye taasisi za Serikali, kuandaa Kanzi-Data ya watumishi wenye utaalamu wa masuala ya ufuatiliaji na tathmini, kuongeza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye ufuatiliaji na tathmini na kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ili kujenga mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ambao utawezesha kufuatilia, kuchambua na kupata taarifa halisi na kwa wakati za utendaji wa Serikali.

**ULINZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA**

42. ***Mheshimiwa Spika***, suala la kulinda na kuhifadhi mazingira limeendelea kuwa moja ya vipaumbele muhimu

vya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais katika hotuba zake mbalimbali ndani na nje ya nchi, amekuwa akisisitiza umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ustawi wa jamii yetu na kwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu ambazo siyo endelevu na rafiki wa mazingira zikiwemo ukataji wa miti hovyo, uvamizi na uharibifu wa mapori tengefu, ukataji wa miti holela kwa ajili ya uchomaji wa mkaa, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na uchomaji moto misitu yetu zimekuwa zikichangia sana uharibifu wa mazingira nchini. Jitihada zinazofanywa na Serikali kuhifadhi mapori yetu ni katika kulinda tunu zilizopo kwenye maeneo muhimu kama vile Loliondo, Ngorongoro, Selou, Ruaha, Katavi n.k.

**Pori Tengefu la Loliondo**

44. ***Mheshimiwa Spika***, Pori Tengefu la Loliondo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 4,000 limekuwa likitumiwa na wananchi kuendesha shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ulishaji wa mifugo na makazi. Serikali kwa upande wake imeendelea kulitumia katika shughuli za uhifadhi na utalii. Aidha, matumizi yasiyo rafiki yamekuwa chanzo cha kuharibika kwa mfumo ikolojia wa Pori hilo.

45. ***Mheshimiwa Spika***, Pori Tengefu Loliondo ni muhimu kwa ajili ya kulinda Mfumo Ikolojia ya Serengeti, ikiwemo maeneo ya mazalia, makazi na mapito ya makundi makubwa ya nyumbu wahamao. Sababu kubwa ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ni kuhifadhi mzunguko wa nyumbu ambao kwa kiasi kikubwa uko upande wa Tanzania na umuhimu wake kama urithi wa dunia. Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko pale ambapo imeonekana mzunguko

huu uko hatarini na hivyo kuhakikisha kuwa unalindwa kikamilifu.

46. ***Mheshimiwa Spika***, maeneo muhimu yanayohitaji kuhifadhiwa kwa lengo la kulinda mzunguko wa nyumbu ni maeneo ya mazalia na mapito kwenye eneo la kilomita za mraba 1,500 za Pori Tengefu la Pololeti. Maeneo mengine muhimu ni vyanzo vya maji ambavyo huingiza maji kwenye mito mikuu mitatu ya Nyabogati, Pololeti yenyewe na Grumeti.

47. ***Mheshimiwa Spika***, uhifadhi wa maeneo haya ni muhimu ili kuinusuru ikolojia ya Serengeti ikiwemo Bonde la Seronera ambako mito hii humwaga maji yake na ndicho kitovu cha utalii ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti. Kadhalika, eneo hilo la Pololeti - Loliondo linalopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, limeendelea kuwa eneo muhimu kwa ajili ya mtawanyiko wa wanyamapori hususan nyumbu, pundamilia na Pofu.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na makazi zimekuwa chanzo cha uharibifu wa ikolojia niliyoielezea ambayo ni muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa hifadhi zetu hususan Serengeti. Vilevile, shughuli hizo zimechangia uharibifu wa uoto wa asili na kusababisha kukosekana kwa malisho na maji, kupungua uwezo wa kiuchumi kwa wafugaji. Aidha, ongezeko la mifugo limesababisha maeneo yote ya vyanzo vya maji na mito kuharibika. Uharibifu huo mkubwa wa mazingira, pia, umekuwa chanzo cha wanyamapori kutoweka.

49. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha uwepo wa matumizi endelevu ya Pori Tengefu la Loliondo, Serikali ilielekeza eneo la kilometa za mraba 1,500 lihifadhiwe na eneo lililobaki la kilometa za mrada 2,500 wananchi waendelee kulitumia kwa shughuli nyingine. Utekelezaji wa

maelekezo hayo ya Serikali umehusisha zoezi la kuwekwa vigingi katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,500 la Pori Tengefu Pololeti - Loliondo.

50. ***Mheshimiwa Spika***, zoezi hili la uwekaji wa vigingi **ambalo limekamilika kwa asilimia 100** halitoathiri maendeleo ya wakazi wa eneo la vijiji 14 vinavyopakana na eneo hilo. Aidha, hakutakuwepo na Kijiji kitakachofutwa na hakuna miundombinu itakayoondolewa kwa kuwa ndani ya eneo la kilometa za mraba 1,500 la Pololeti hakuna miundombinu yoyote.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imesimamia kwa umakini mkubwa zoezi la uwekaji vigingi kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 ambalo ni muhimu kwa ikolojia ya Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Halikadhalika, Serikali imeendelea kushirikiana na wananchi wa Loliondo katika kuboresha malisho ya mifugo, uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa majosho pamoja na miundombinu ya kunyweshea mifugo kwenye eneo la kilometa za mraba 2,500.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** pia**,** ninaielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na wadau wengine kuhakikisha kuwa Sheria ya Ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999 inatumika ipasavyo kutenga na kuweka mipaka ya vijiji. Serikali kwa kuzingatia matakwa ya wananchi hasa maeneo ya malisho kwenye vijiji 14 vilivyopo karibu na Pori Tengefu la Poloreti itaweka utaratibu utakaopangwa kwa pamoja baada ya kukamilisha zoezi la utambuzi wa mifugo kwenye vijiji husika kwa lengo la kuwezesha kuhudumia mifugo iliyopo ndani ya eneo hilo.

**Hifadhi ya Ngorongoro**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** tangu kuanzishwa kwa matumizi mseto ya ardhi, takriban miaka 60 iliyopita, usimamizi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro umeshindwa kutimiza lengo la kuleta uwiano baina ya uhifadhi, ukuzaji wa utalii na maendeleo ya jamii kutokana na changamaoto mbalimbali. Hali hiyo imechangiwa na changamoto nyingi za kiuhifadhi na maendeleo ya jamii hususan ongezeko la idadi kubwa ya watu na mifugo, makazi holela na shughuli za binadamu. Kwa mfano, mwaka 1959 wakati Hifadhi hiyo inaanzishwa kulikuwa na watu takriban 8,000 na mifugo 161,000. Lakini hadi sasa idadi ya watu inakadiriwa kuwa takribani 110, 000 na mifugo zaidi ya 1,000,000. Ni jukumu la Serikali kuweka miongozo itakayowezesha maisha ya watu na uhifadhi kuwa endelevu kwa maslahi ya Taifa.

54. ***Mheshimiwa Spika***, changamoto nyingine ni kuendelea kudorora kwa ustawi wa maisha ya wenyeji wa Ngorongoro katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo elimu, afya, uchumi, usalama wa chakula na lishe, ufinyu wa vyanzo mbadala vya mapato kwa jamii, makazi duni, kukosa haki ya msingi ya kikatiba ya kumiliki na kutumia ardhi kwa ajili ya maendeleo yao kwa sheria zilizopo, pia kumejitokeza kubadilika kwa uoto wa asili na kuenea kwa mimea vamizi. Hivyo, kuendelea kuwepo kwa mfumo uliopo, kunaathiri ustawi endelevu wa maliasili ambazo ndio chanzo kikubwa cha mapato ambayo hugharamia shughuli za maendeleo na ustawi wa watanzania.

55. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia hali hiyo, Serikali kwa nyakati tofauti ilichukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto za usimamizi wa hifadhi ikiwemo kufanya tathmini ya kina tangu mwaka 2017 hadi mwaka 2021 kwa lengo la kutatua changamoto za mfumo wa matumizi mseto ya ardhi. Kutokana na tathmini hiyo, Serikali iliamua kutumia mapori Tengefu ya Handeni na Kitwai yaliyopo katika Wilaya za Simanjiro, Handeni na Kilindi kwa ajili ya wananchi wa

Ngorongoro kuhamia na kuendeleza maisha yao na kujitafutia shughuli mbalimbali za uchumi.

56. ***Mheshimiwa Spika***, sababu ya kutumia maeneo ya Handeni na Kitwai ni pamoja na kufaa kwa ufugaji na kilimo; mwingiliano wa kimila, kitamaduni na desturi katika ya jamii iliyopo Handeni na Kitwai na jamii ya wafugaji wa Ngorogoro na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo zinafanana sana ambapo shughuli kuu ni ufugaji.

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha maeneo hayo yanakidhi makusudio yaliyotarajiwa, Serikali imeendelea kujenga miundombinu muhimu katika eneo la Msomera ikiwemo upangaji na upimaji wa viwanja vya makazi na mashamba na ujenzi wa nyumba 500 za wakazi ambapo ujenzi wa nyumba 103 umekamilika na ujenzi wa nyumba 400 unaendelea kupitia JKT. Vilevile, huduma za umeme na maji tayari zinapatikana na ujenzi wa shule ya msingi na sekondari umekamilika. Ujenzi wa miundombinu ya afya, majosho na barabara unaendelea.

58. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa za eneo la Msomera lililopo Handeni kiuchumi na kijamii kupitia vikao vingi na wananchi wa eneo la Ngorongoro wakiwemo viongozi wa mila (Laigwanak), waheshimiwa madiwani, watendaji wa kata na vijiji (WEO na VEO) wawakilishi wa akinamama, vijana na wadau wengine. Hadi sasa, kumekuwa na mafanikio makubwa katika kusimamia utekelezaji wa zoezi hilo ambapo Serikali imeendelea kuhamasisha na kuandikisha zile kaya ambazo zipo tayari kuhama kwa hiari.

59. ***Mheshimiwa Spika***, zoezi la kuandikisha wakazi wanaoomba kuhama kwa hiari linaendelea vizuri. Aidha, hadi kufikia tarehe 09 Juni 2022, jumla ya kaya 293 zenye watu 1,497 zimejiandikisha.

60. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wakazi wanaohama wanakuwa na maisha bora zaidi katika makazi mapya Msomera, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia kutoa motisha mbalimbali kwa wakazi hao kama ifuatavyo:-

**Moja:** Kila Kaya inayoondoka inapewa fidia ya nyumba aliyokuwa anaishi;

**Mbili:** Kaya zote zinazohamia Msomera kwa hiari zinapatiwa nyumba zenye vyumba vitatu zilizojengwa kwenye eneo la ekari 2.5, godoro, tochi, na ndoo;

**Tatu**: Kila kaya inapewa shamba lenye ukubwa wa ekari tano na zitakabidhiwa hati za kumiliki ardhi kwa ajili ya eneo la nyumba na shamba. Pia lipo eneo lingine huru la kuchungia;

**Nne**: Kila kaya inapewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzia maisha kwenye makazi mapya; na

**Tano:** Kila kaya inapewa mahindi magunia mawili kwa kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya kujikimu katika kipindi cha mpito wakati wakazi wakijiandaa na maandalizi ya kilimo.

61. ***Mheshimiwa Spika***, upendo huo uliooneshwa na Mheshimiwa Samia, Rais wetu haunabudi kupongezwa na kila mwenye kuitakia mema nchi hii. Hata hivyo, utaratibu huu ni maalumu kwa Ngorongoro pekee. Leo tarehe 30 Juni, 2022 kaya nyingine 25 zenye jumla ya watu 115 zinatarajiwa kusafiri kwa hiari kuelekea Msomera na kuendelea na maisha yao kama kawaida. Nitumie nafsi hii kuwapongeza wananchi wote walioridhia kuhama kwa hiari. Tarehe 23 Juni 2022 nilitembelea Ngorongoro na nilipata fursa ya kuwaaga wananchi wanaohama kwa hiari kutoka hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera. Aidha, siku hiyo hiyo,

nilitembelea eneo la Msomera lililopo Wilaya ya Handeni na kujionea wananchi waliohamia katika eneo hilo wakiendelea na shughuli zao kwa furaha ambapo waliishukuru sana Serikali na Mheshimiwa Rais kwa kuwaandalia makazi bora katika eneo hilo. **Mheshimiwa Spika kwa ridhaa yako ninaomba tuwasikilize**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa viongozi na watendaji kuendelea kuelimisha, kuhamasisha na kuwashirikisha wananchi na wadau wengine hususan wenyeji katika utekelezaji mzuri unaoendelea wa zoezi hilo.

**Upandishwaji Hadhi wa Maeneo ya Mapori Tengefu kuwa Mapori ya Akiba**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** rasilimali za wanyamapori ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, hususan katika kukuza utalii na hivyo kuongeza pato la Taifa. Kwa msingi huo, mpango wa Serikali kupandisha hadhi baadhi ya mapori tengefu kuwa mapori ya akiba ni katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali zilizopo katika mapori hayo kwa uhifadhi endelevu.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, kutangazwa kwa eneo lolote kuwa Pori la Akiba hufanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufuata taratibu zilizowekwa kisheria ikiwemo kufanya tathmini ya kina ya umuhimu wa eneo hilo katika uhifadhi na ushirikishwaji wa wananchi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa za maeneo husika.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini hiyo na ushirikishwaji wa wananchi husaidia Serikali kufanya maamuzi ya iwapo kuendelea na utaratibu wa kupandisha hadhi au la. Hivyo, naomba niwahakikishie wananchi wa maeneo husika ikiwemo Loliondo kwamba utaratibu wa kupandisha hadhi maeneo ya mapori hayo kuwa mapori ya akiba utasubiri mapitio ya pamoja kati ya Serikali na wananchi. Hivyo, Wizara

isianze zoezi hilo hadi wananchi watoe maoni yao kwa maslahi ya pande zote.

**KILIMO**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294 katika mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 954. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 224 na limelenga kwenye maeneo yafuatayo: Utafiti wa kilimo, Uzalishaji wa mbegu, Umwagiliaji, Ujenzi wa maghala na Kuimarisha huduma za ugani.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Serikali ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 (Agenda 10/30); kuongeza mauzo nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 hadi kufikia Dola za Marekani Bilioni 5 mwaka 2030; kupunguza umaskini kwa zaidi ya asilimia 50 kutoka asilimia 28 kwas asa hadi chini ya asilimia 14 ifikapo 2025.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo hayo Serikali imepanga kuimarisha utafiti; kutoa ruzuku ya mbegu za alizeti, ngano na miche ya chikichi; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo; kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo utakaowezesha upatikanaji wa pembejeo kwa mfumo wa ruzuku pindi inapotokea athari za kiuchumi na kuanza kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/2023.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la bajeti kwa mwaka 2022/2023 linatarajiwa kuimarisha usalama wa chakula na lishe na hivyo kupunguza mfumuko wa bei ya chakula nchini; kuongeza eneo la umwagiliaji; kuongeza upatikanaji wa ajira kwa vijana na wanawake katika kilimo zitakazofikia milioni moja ifikapo mwaka 2025. Manufaa mengine ni kuhakikisha

upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa za kilimo kufikia asilimia 100 ifikapo 2030.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za kupanda kwa bei ya mbolea duniani, Serikali itaimarisha mfumo wa utoaji ruzuku ambapo tunatarajia kutumia Shilingi Bilioni 150 kutoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote. Kwa kipekee mfumo wa utoaji wa ruzuku utawalenga wazalishaji wa ndani. Aidha, kwa kipekee makampuni ambayo hayataungana na Serikali katika mfumo huu Serikali hatutosita kuwafutia leseni ya kuendesha biashara ya mboloea nchini.

**MAELEKEZO MAHSUSI**

71. ***Mheshimiwa Spika***, ni dhahiri kuwa hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimekuwa na zinakusudia kuleta matokeo chanya na ya haraka kwenye nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa msingi huo, nami ningependa kusisitiza na kuelekeza utekelezaji wa masuala yafuatayo: -

**I: Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na mamlaka mbalimbali za Serikali inazungumza**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imepata mafanikio mbalimbali katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA, ikiwemo kuunganisha taasisi zaidi ya 700 katika mfumo mmoja wa malipo GePG. Hivi sasa, Serikali inaweza kuona na kupata taarifa za makusanyo yote yaliyokusanywa kwenye taasisi zake kupitia mfumo uliounganishwa na mifumo mingine kama vile MUSE, GAMIS, TANePS, ERMS, HCMIS, LGRCIS, mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na mifumo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

73. ***Mheshimiwa Spika***, licha ya mafanikio hayo makubwa Serikali imejenga mfumo maalum unaojulikana kama *Government Enterprise Service Bus* (GovESB) kwa ajili ya kuwezesha mifumo mbalimbali ya Mamlaka na Taasisi za Serikali kubadilishana taarifa na kuzungumza. Kwa msingi huo, ninaelekeza **Wizara ya Fedha ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na wadau wengine muhimu kutekeleza yafuatayo**: -

**Moja:** Kuhimiza taasisi za umma kuunganisha mifumo yao ya TEHAMA kupitia mfumo huu maalum;

**Mbili:** Kusimamia ujenzi wa mfumo wa *Universal Billing System* utakaotumiwa na taasisi ambazo hazina uwezo wa kujenga mifumo yao; na

**Tatu:** Kuhakikisha taasisi za umma zinajielekeza zaidi katika matumizi ya mifumo shirikishi pale ambapo taratibu za utendaji kazi zinafanana badala ya kila taasisi kujenga mfumo wake. Hakikisheni mifumo yote mipya ya TEHAMA inajengwa kwa kufuata Sheria, Taratibu, Kanuni, Viwango na miongozo inayosimamia matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa Serikali.

**II: Viongozi na Watendaji wa Serikali kuisemea na kutangaza mafanikio ya Serikali kwenye maeneo yao na sekta husika**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya wanazuoni wamewahi kusema kuwa **uongo ukisemwa mara nyingi hugeuka kuwa ukweli**. Nimeamua kurejea kauli hiyo kutokana na ukweli kwamba uzoefu wa mwaka mmoja wa uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaonesha kuwa yapo mafanikio lukuki tuliyoyapata kama nchi katika kipindi hicho. Hata hivyo, licha ya ukweli huo bado wananchi hawajaelezwa ipasavyo

na wakati mwingine tumeacha upotoshaji kufanywa bila kusahihishwa au kuchelewa sana kusahihisha.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua kuwa ni jukumu letu viongozi na watendaji wote kuhakikisha wananchi wanaelezwa kuhusu shughuli zinazofanywa na Serikali, mafanikio na changamoto zilizopo ninaelekeza viongozi na watendaji wote kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kupata taarifa za Serikali kuhusu juhudi mbalimbali za kuwaletea maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa mujibu wa ibara ya 18 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**III: Mpango wa kutoa Elimumsingi Bila Ada**

76. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake na dhamira njema ya kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 kuhusu Serikali kutoa Elimumsingi Bila Ada kwa ngazi ya shule za msingi na sekondari yenye kulenga kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu, mahudhurio na ufaulu.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utekelezaji wa mpango huu, Waheshimiwa Wabunge wamelalamikia kuwepo utitiri wa michango shuleni. Aidha, Serikali kupitia waraka wa elimu na 5 wa mwaka 2015 na waraka wa elimu namba 6 wa mwaka 2015 imetoa maelekezo bayana kuhusu utekelezaji wa Elimumsingi Bila Ada ikiwemo matumizi ya fedha za utawala ambazo hutolewa HAZINA na kupelekwa moja kwa moja katika akaunti za shule za msingi na sekondari kwa ajili ya Vifaa vya kufundishia na kujifunzia, Ukarabati, Uendeshaji wa mitihani ya ndani na Utawala.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** asilimia 10 ya fedha hiyo pia hutumika kugharamia huduma za umeme, maji na ulinzi.

Hivyo basi, ninaagiza kuwa TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kufuatilia matumizi na upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha hizo pamoja na kuhakikisha hakuna michango holela inayotozwa kwa wanafunzi. Aidha, kuanzia sasa hakikisheni maelezo ya kujiunga na shule za umma (yaani *Joining Instructions*) yanahakikiwa na kupewa idhini na Katibu Tawala wa Mkoa husika kwa kushirikiana na Maafisa Elimu wa maeneo husika.

**IV: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022**

79. ***Mheshimiwa Spika*,** eneo la mwisho ambalo ningependa kulitolea msisitizo ni utekelezaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Kama mnavyofahamu, tarehe 23 Agosti 2022 imepangwa kuwa siku ya Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022. Zoezi hilo lilitanguliwa na Operesheni ya Anwani za Makazi ambayo utekelezaji wake umefikia **asilimia 95** na Serikali imefanikiwa kukusanya taarifa na kutoa anwani za makazi zaidi ya milioni 12**.**

80. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi ninaelekeza kama ifuatavyo: -

**Moja**: Taasisi zote zenye dhamana ya masuala ya ardhi na makazi kuhakikisha zinakuja na mikakati thabiti ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyoainishwa wakati wa utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi pamoja na kutoa miongozo ya namna bora ya kushughulikia changamoto za watanzania wenzetu kuishi katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria ili kuhakikisha wananchi wote wananufaika na fursa zitokanazo na zoezi hilo;

**Mbili**: Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhakikisha kuwa Mpango wa Uendelezaji wa Mfumo (*System Sustainability Framework*) unaotoa

mwongozo wa shughuli zote za anwani za makazi zitakavyofanyika unatumika vizuri ili kufanya zoezi hili kuwa na thamani wakati wote;

**Tatu**: Viongozi katika ngazi zote hususan kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wahakikishe kuwa jamii inaendelea kuelimishwa ili kujua manufaa sanjari na kulinda miundombinu ya anwani za makazi kwenye maeneo yao;

**Nne**: Wizara zote, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa endeleeni kushughulikia changamoto zote zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Operesheni Anwani za Makazi na kuhakikisha zoezi hilo linakuwa endelevu; na

**Tano**: Uhakiki wa majina ya mitaa katika vibao uendelee kufanyika ili kujiridhisha na usahihi wake na muonekano wake.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yanaendelea vizuri na yamefikia asilimia 87. Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu hususan mnaporejea kwenye maeneo yao ya uwakilishi kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye zoezi hilo muhimu. Vilevile, nitoe wito kwa watanzania wote kujiandaa kuhesabiwa ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Makarani wa Sensa na viongozi wetu kwenye maeneo tunayoishi.

**MICHEZO**

82. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa michezo nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa kupaisha mchezo wa soka nchini na kuifanya ligi ya Tanzania kuwa kivutio kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

83. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ninaipongeza Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 maarufu **Serengeti Girls** kwa kufuzu kushiriki michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika Oktoba mwaka huu nchini India. Tunawatakia kila la heri wawakilishi wetu hao ambao wataungana na Morocco na Nigeria kuiwakilisha Afrika na kukamilisha idadi ya timu 16 zitakazoshiriki fainali hizo za Dunia zikiwa ni fainali za saba tangu michuano hiyo ilipoasisiwa mwaka 2008.

84. ***Mheshimiwa Spika***, naipongeza pia Timu ya Taifa ya Walemavu ya Mpira wa Miguu (Tembo Warriors) kwa kufuzu kucheza Kombe la Dunia mwezi Oktoba 2022 nchini Uturuki. Nitoe wito kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana kwa karibu na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) kuwezesha maandalizi mazuri kwa timu zote mbili kuelekea mashindano hayo ya Dunia ili tukashindane na kuitangaza vema Tanzania.

85. ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kwa upande wa michezo niwapongeze sana **Dar Young Africans** (Wananchi) kwa kuibuka vinara wa Ligi Kuu ya NBC kwa msimu wa 2021/2022. Hongereni sana wananchi, mmekuwa na msimu mzuri sana na mmestahili kuibuka mabingwa. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa matukio yaliyonivutia wakati wa shamrashamra za Ubingwa wa wananchi ni kitendo chao cha kukumbuka kuitangaza Tanzania kupitia **Royal Tour** na kuhamasisha ushiriki wa **Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022**, kama ambavyo klabu ya soka ya Simba ilivyoanzilisha kuitangaza Tanzania kwenye medani za soka za kimataifa kupitia jezi zao kuandikwa **VISIT TANZANIA.** Niendelee kutoa wito kwa vilabu na makundi ya watanzania wanaosafiri nje kuhakikisha wanatumia jezi zetu zenye kubeba jumbe au ajenda za kitaifa kwani **jukumu la kuitangaza Tanzania na ajenda zake za kitaifa ni letu sote.**

**HITIMISHO**

86. ***Mheshimiwa Spika***, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, niwatakie safari njema Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnaporejea majimboni kwenu. Niwaombe mtakapokuwa huko majimboni muwaeleze wananchi mambo yaliyojiri hapa Bungeni wakati wote wa Mkutano wa 7 wa Bunge hili la 12, matarajio yetu kwao na kuwasihi kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita kwenye jitihada zake za kuwawekea mazingira wezeshi ya kujikwamua kiuchumi.

87. **Mheshimiwa Spika,** niwashukuru pia, watendaji wa Serikali ambao weledi na ufanisi mkubwa waliouonesha umekuwa chachu katika kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu. Vilevile, niwashukuru wanahabari kwa kufikisha habari za Mkutano huu kwa wananchi. Kipekee, nivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili bila kuwasahau madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa bungeni. Pia, nimshukuru Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri mliyotupatia ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri kwa kipindi chote cha miezi mitatu. Ninawatakia safari njema.

88. ***Mheshimiwa Spika*****,** tunatarajia kwamba tarehe 10 Julai, 2022 kutegemea mwandamo wa mwezi, kutakuwa na sikukuu ya Eid El Hajj. Nitumie fursa hii kuwatakia ndugu zetu Waislamu na Watanzania wote nchini maadhimisho mema ya sikukuu hiyo.

89. ***Mheshimiwa Spika*****,** baada ya maelezo hayo, sasa napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu liahirishwe hadi tarehe 13 Septemba 2022 siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu Jijini Dodoma.

90. ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tupige yale makofi yetu ambayo tumekubaliana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu!

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliimbwa na Brass Band)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge sasa naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Bunge nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyotueleza mambo mengi ambayo tumeweza kufanya Bunge hili ambalo tumekaa muda mrefu zaidi, pia tunakupongeza kwa maelekezo na maagizo ambayo umetoa kwa upande wa Watendaji wa Serikali katika mambo mbalimbali nao tuwatakie kila la heri katika kutekeleza yale ambayo umeyaagiza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mambo machache kabla sijaahirisha ninayo mambo matatu; la kwanza kabisa ni hili ambalo nadhani kuna Wabunge pengine hawajanielewa vizuri nilivyomwambia Mheshimiwa Mpina hoja yake haiwezi kutumia Kanuni ya 76 halafu akatupeleka kwenye Kanuni ya 70.

Kanuni ya 76 inatueleza kwamba Mbunge anaweza akasimama akaomba Mwongozo wa Spika na wakati huo kama kuna Mbunge anayesema basi atanyamaza.

Waheshimiwa Wabunge tusikilize, anaweza akawa alikuwa pengine Mbunge mwingine anachangia akimaliza tu kama hakuna aliyesimama yeyote na mimi pia sizungumzi na sijasimama basi Mbunge anaruhusiwa kusimama na kusema Mwongozo wa Spika.

Sasa ukitumia Kanuni hii ya 76 inataka uwe unaomba Mwongozo juu ya jambo ambalo limetokea mapema Bungeni. Kwa maana hiyo humu tulishatoa maelekezo mapema maana yake siku ya leo.

Kanuni ya 70 mtakumbuka wakati akitoa maelezo yake kuhusu kutokusema uongo Bungeni na nilipoanza kumsikiliza hoja yake akataja tarehe 18 Mei, 2022 na akataja pia tarehe 24 Juni, 2022; katika hizo siku mbili hakuna siku ambayo ni leo, leo ni tarehe 30 Juni, 2022.

Sasa matumizi ya Kanuni ya 70, maana sasa nimepata vikaratasi vingi hapa mtu akizungumza uongo ni mazingira gani fasili ya (3) inasema; Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka Kuhusu Utaratibu na baada ya kuruhusiwa na Spika kudai kwamba Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya suala alilokuwa analisema Bungeni siyo alilokuwa amelisema, alilokuwa analisema, maana yake wakati akiwa anazungumza kasema jambo la uongo ndiyo Mbunge mwingine anasimama kuomba kuhusu utaratibu. Fasili ya (2) hiyo niliyowasomea ni fasili ya (3); fasili ya (2) inasema Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa au lililoandikwa na vyombo vya habari.

Sasa niwasomea hii fasili ya (3) ili muelewe kwamba kama hizi tarehe anazozisema Mheshimiwa Mpina ndipo hayo anayoyasema yalisemwa uongo huwezi kutumia hata Kanuni ya 70 kwa siku kama leo kwa sababu unapaswa useme siku hiyo ambayo mtu anasema siyo tu siku hiyo wakati huo akisema ndiyo useme anasema uongo na ukishasema huyo anasema uongo ni kazi yako wewe kikanuni kuthibitisha kwa nini anasema uongo, siyo kazi yake yeye kujitetea, ni kazi yako wewe kuthibitisha uongo wake ni wa aina gani.

Kwa mazingira hayo ndiyo maana jambo la kusimama kwenye Kuhusu Utaratibu hasa kwa Kanuni ya 70 inataka uliseme wakati mtu anapochangia. Sasa nieleze vizuri hapa Mheshimiwa kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Mpina mara ya mwisho jambo hili limezungumzwa humu ndani Waziri alikuwa hayupo hapa mbele kwa sababu akiwa hapa mbele ni dhahiri kanuni zetu haziruhusu mtu kusimama kuanza kusema Waziri hapo mbele pengine amesema uongo. Kwa hiyo, huwezi kusimama kuhusu utaratibu kanuni zetu haziruhusu.

Lakini Waziri anapokuwa anachangia hoja ya Waziri mwingine ni mchangiaji mwingine tu kama Mbunge mwingine, kwa hivyo unayo haki ya kusimama. Kwa hiyo

Mheshimiwa Mpina alikuwa nayo hiyo haki Mbunge mwingine akichangia kama yeye aliona hicho anachokisema ni uongo, alikuwa na nafasi hiyo wakati Mbunge huyo akichangia. Kwa sababu hakuitumia nafasi hiyo na kanuni zetu zimewekwa hivi kwa nia njema tu Waheshimiwa Wabunge, siyo kwamba msiende kufanya utafiti, hapana, lakini maana yake mambo yatakuwa hayaishi kwanini? Kwa sababu inawezekana hoja ikapita hapa, Wabunge wakachangia, halafu Bunge likawalimeshafanya maamuzi na hakuna nafasi ya kwenda kufungua maamuzi ambayo Bunge lilishayafanya na ndiyo utaratibu ambao kanuni zetu zinafanya hivyo ili tuweke mazingira ambavyo jambo linaweza kufika mahali na Bunge likafanya maamuzi.

Kwa hiyo, kwa kuwa Bunge haliwezi kurudi nyuma kwenda kufungua maamuzi yake isipokuwa kwenye kubadilisha sheria zile tunazotunga na zenyewe kwa utaratibu maalum basi mazingira hayo ndiyo maana kanuni zetu ziko hivyo, isingekuwa hivyo maana yake mtu angeweza kusema hata mwaka jana fulani alidanganya halafu tuanze kushughulika nalo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mlielewe hivyo jambo hilo.

Sasa nilisema mambo matatu; jambo la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu amelieleza kwa kirefu sana hapa na mimi ningependa kusisitiza jambo hili la Loliondo na Ngorongoro ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunavyotoka hapa tunaenda majimboni, tuwe tayari kujibu maswali ya wananchi kwenye majimbo yetu kuhusu hoja hii, na Mheshimiwa Waziri Mkuu amefafanua kwa kirefu sana sina haja ya kufafanua, tutoke hapa na taarifa zilizo sahihi kuhusu Loliondo hakuna mwananchi anayehama kwa hiari hayupo, kwa nini kwa sababu kule inawekwa tu mipaka ya eneo ili mwananchi ajue tunaishia wapi huko ni Loliondo. *(Makofi)* Loliondo inawekwa mipaka na ndiyo maana huwa inabidi msikilize yakiwa yanasemwa maneno hapa mbele, Loliondo ni mipaka, hakuna mwananchi anahama, kama

anahama kwa hiari yake ni kama mimi ninavyohamia Dodoma na mwingine anavyohamia sehemu nyingine, lakini siyo kwa maana ambayo utaratibu ambao Serikali imeweka ya yeye kuhamia mahali, ila kama anahama kama mimi na wewe, wananchi wote hapa nchini wanahaki ya kuishi popote. Kwa hiyo, hata yeye anaruhusiwa kuhama, lakini Serikali haina utaratibu yaani haujaweka kuhama wala kuhamishwa upande wa Loliondo. *(Makofi)*

Upande wa Ngorongoro watu wanaohama na sisi ndiyo watalaamu wa kiswahili, wale watu wanahama kwa hiari, hawahaamishwi kwa hiari, hayo ni maneno mawili tofauti, wanahama kwa hiari hawahamishwi kwa hiari. Pamoja na kwamba kule kuhama kwao Serikali inaenda mbali zaidi kwa maana ya kupeleka usafiri kwa ajili yao, kwa ajili ya mifungo, kwa ajili ya vitu vyao wanavyotaka kuhama navyo na kwamba Serikali imeshatafuta eneo, imejenga na nyumba, imeweka miundombinu, sasa hiyo isipelekee kwamba Serikali inahamisha watu Ngorongoro, watu wanahama kwa hiari. *(Makofi)*

Hivyo tutumie maneno ya kiswahili vizuri kwa sababu tusipofanya hivyo mtu akitafsiri kiingereza ataita *eviction* na ndicho kinachosemwa, sasa *eviction* ni *either* kuhamishwa na kuhamishwa maana yake kunaweza kuwa pande mbili, unahamishwa kwa hiari au unahamishwa kwa nguvu, ama kufukuzwa lile neno *eviction* lile neno *eviction* maana yake kufukuzwa, hamna mtu anafukuzwa Ngorongoro, watu wanahama kwa hiari isipokuwa Serikali imetengeneza utaratibu wa yule anayehama imemuwekea utaratibu. Kwa hiyo, sisi twende huko majimboni tukayaseme mambo haya kwa ufasaha, tusipotoshe sisi kama Wabunge. *(Makofi)*

Nadhani hilo limeeleweka vizuri na pia ni vizuri kwa sababu mara nyingi huwa tunatumia hata maeneo sisi Watanzania tunachangamoto hiyo kuna maeneo ambayo makabila fulani yanakuwa makubwa kuliko mengine, kwa

hiyo watu wanafikiria eneo fulani ni la kabila fulani, sasa hata huku Ngorongoro wanaohama kwa hiari siyo Wamasai peke yao, hata wanaohama kwa hiari Ngorongoro si Wamasai peke yao, ni pamoja na jamii zingine zilizopo kule Ngorongoro wanaohama kwa hiari. *(Makofi)*

Kwa hiyo isionekane kana kwamba hao wanaohama kwa hiari ni kabila moja, hapana, yapo makabila mengi kule na yote yanaruhusiwa kuhama kwa hiari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hilo lilikuwa jambo la pili, jambo la tatu; Bunge letu hapa nilikuwa nawasikiliza Waheshimiwa Wabunge wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anaitaja tarehe ile ambayo tutarejea kwa ajili ya Bunge linalofuata naona watu wamehesabu siku hapo na nini, lakini msingi wake mkubwa ni kwamba tunayo Sensa mbele yetu. Sensa itakuwa siku ya tarehe 23 Agosti, 2022 Waheshimiwa Wabunge wote tunatarajiwa kuhesabiwa kwenye maeneo yetu ya uwakilishi. Kwa sababu kama tunavyowasisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa na kwamba kila mtu ahakikishe yeye ahesabiwe na jirani yake ahesabiwe na mwingine yeyote ahesabiwe ili tunapokuwa na takwimu ziwe ni takwimu halisi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Sasa hata wewe Mbunge ukija kuhesabiwa hapa Dodoma halafu unawazungumzia wananchi wako hapa nilitaka kutaja Liwale, lakini Liwale kwa sababu wanaenda Jimboni, kwa hiyo naweza kumtumia yeye kama mfano. Sasa wananchi wako wa Liwale hiyo namba moja ya mtu mmoja wewe utakuwa umehesabiwa huku kule wataonekana Liwale wapo idadi fulani wakati wewe upo huku. Kwa hiyo, kahesabiwe na wewe kule ili maendeleo yanapoletwa na Serikali na wewe mwakilishi uwe umehesabika kwenye eneo lako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana kushiriki hili zoezi na ndiyo maana ratiba hii imesogea mbele ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge kwanza kwenda kuhamasisha wananchi kushiriki Sensa, lakini pia ninyi

wenyewe kushiriki kuhesabiwa kwenye maeneo yenu ya uwakilishi na tunawatakia kila heri katika hilo na tunaamini mambo yataenda vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kulisema jambo hili la mwisho sasa ni...

Haya hapa nakumbushwa sasa hili halikuwepo kwenye ile orodha, lakini Waheshimiwa Wabunge nakumbushwa hapa na Katibu kwamba Bunge lijalo hili ambalo ameitaja tarehe Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nami nitaitaja punde uchaguzi wa wale Wabunge wanaoiwakilisha Tanzania kwenye Bunge la Afrika Mashariki utafanyika. Kwa hiyo, utafanyika uchaguzi Bunge lijalo katika ratiba yetu ile tutakayokuwa nayo tutapanga siku moja tufanye uchaguzi huo.

Kwa hiyo, tangazo hili ni kwa ajili ya Watanzania wajue lakini pia watatangaziwa na vyama vyao kwa sababu kama Katiba yetu inavyosema hawa watatokana na vyama husika. Kwa hiyo, vyama vitapelekewa taarifa uchaguzi utafanyika mwezi wa Septemba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niahirishe Shughuli za Bunge mpaka siku ya tarehe 13 Septemba, 2022 siku ya Jumanne saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.05 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 13 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*